Kal 3000

# UAMILISHI DHIMA KATIKA SENTENSI ZA LULOOGOLI: MTAZAMO WA SINTAKSIA FINYIZI

TASNIFU

YA

ASIKO BEVERLYNE AMBUYO

ILIYOANDIKWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Asiko, Beverlyne
*Uamilishi dhima katika sentensi za*
08/322526

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya kupata shahada katika chuo kikuu chochote.

..........................................................................................

**ASIKO BEVERLYNE AMBUYO**

Kazi hii imetayarishwa chini ya usimamizi wetu na kutolewa kwa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa chuo kikuu cha Kenyatta.

..........................................................................................

**DAKTARI ALICE MWIHAKI**

..........................................................................................

**DAKTARI MBATHA MATHOOKO**

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# SHUKRANI

Ninawashukuru nyote ambao mlijitolea kwa moyo mkunjufu kunisaidia kuiandika kazi hii. Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Mwihaki Alice na Dkt. Mbatha Mathooko kwa mwongozo mwema. Kwa wanafunzi wa darasa langu, Ahsante; kwa Sheila, ahsante kwa uvumilivu wako kuipiga chapa kazi hii. Mungu awabariki nyote na hata wale ambao walichangia ufanisi huu kwa njia moja au nyingine.

## TABARUKU

Kwa Walter na Rachel, Mungu awape hekima na maarifa.

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| KP | - | Kirai Patanishi |
| KT | - | Kirai Tenzi |
| KN | - | Kirai Nomino |
| N | - | Nomino |
| T | - | Kitenzi |
| ha | - | Hamishe |
| KE | - | Kirai Elezi |
| E | - | Kielezi |
| P | - | Kipatanishi |
| SF | - | Sarufi Finyizi |
| SH | - | Shamirisho |
| KSH | - | Kirai Shamirishi |
| KH | - | Kirai Kihusishi |
| KB | - | Kirai Kibainishi |
| KV | - | Kirai Kivumishi |
| V | - | Kivumishi |


KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## MAELEZO YA DHANA MUHIMU

**Dhima**: Uhusiano wa kisintaksia baina ya virai nomino na kiarifu katika sentensi moja.

**Fundo**: Pahala katika kielelezo matawi, ambapo kirai hujigawa ili kutenganisha vijenzi vyake.

**Idadishi ya Majopo**: Urari wa maneno ya kileksia na kategoria za kisarufi.

**Kanuni**: Sheria za kijumla ambazo hufaa kutawala lugha zote za binadamu

**Hamisho:** Kijenzi kilicho hama.

**Muungano**: Hii ni hatua ya kuunda vipashio vikubwa zaidi kutokana na kuambatanisha majopo ya kisarufi.

**X Baa**: Hii ni nadharia inayojaribu kufafanua muundo wa kirai kwa ujumla

**Shamirisho**: Kiungo cha uamilifu wa kisintaksia ambacho huungana na kiarifu ili kuunda kiungo kikubwa zaidi na huja baada ya kiarifu.

**Shamirishi**: Hii ni kategoria ya kirai ambayo hutumiwa kuanzisha vishazi tegemezi kama vile iwapo, ikiwa na ijapokuwa miongoni mwa mengine.

**Ufungami**: Huuleza uhusiano baina ya pronomino, anafora, na visabiki vyao.

**Ufundani**: Kanuni ambayo huzingatia kikwazo cha uhamisho wa maumbo kutoka pahala fulani kuenda pengine katika uhamisho wa sintaksia.

**Uhamisho**: Utaratibu wa kipashio kusonga kutoka pahali pa awali hadi pengine katika sentensi.

**Uhusika**: Amali ya pronomino au nomino zingine kwa namna ambavyo zinaweza kupewa hadhi ya kiima au yambwa ya kiarifu.

**Utawala:** Uhusiano baina ya neno kuu yaani neno tawala na shamirishi katika kitenzi.

**Utegemezi Muundo:** Kanuni inayohitaji mahusiano ya vipashio mbalimbali vya sentensi na sifa zake, yawe ya kimuundo, kulingana na kategoria za maneno.

**Vigezo:** Ni hali bayana zaidi ambazo zinaweza kutofautisha lugha moja na nyingine.

# IKISIRI

Utafiti huu unaamilisha dhima kupitia muundo na uhamisho wa katika sentensi za Luloogoli. Dhima inabainika kupitia uhusiano wa kisintaksia baina ya virai nomino na kiarifu katika sentensi moja. Dhima zilizoshughulikiwa ni zile za kiima na shamirisho, pamoja na kanuni bia na kanuni bayana zinazotawala matumizi.

Misingi ya kinadharia ya utafiti huu ni Sintaksia Finyizi kwa mujibu wa Chomsky (1995) aliporahisisha hatua changamano zaidi zilizokuwepo kwenye vijinadharia sita vya Utawala na Ufungami. Sintaksia Finyizi inatambua hatua tatu muhimu idadishi ya maneno kupitia majopo ya kisarufi muungano wa maumbo ili kuunda sentensi sanifu, na uhamisho wa vijenzi hivyo katika kugeuza muundo wa sentensi. Data ilikusanywa nyanjani na maktabani; kupitia kwa vitabu mahsusi vya Luloogoli na mazungumzo mahsusi. Mbinu ya kusampuli data kwa lengo maalum ilitumiwa ili kupata data iliyokuwa ikidhihirisha dhima mahsusi.

Uhamisho wa dhima hizi umeelezwa na kudhihirishwa namna unavyotokea kwa kutumia michoro matawi, utafiti huu umeelezwa kwa sura tano. Ya kwanza inashughulikia maswala msingi na nadharia ya utafiti, ikifuatiwa na maelezo ya vijenzi vya sentensi za Luloogoli. Sura ya tatu inaangazia wazi zaidi na kubainisha dhima katika sentensi. Taratibu za uhamisho na kanuni zinazotawala uhamisho wa dhima hizi umeelezwa kwenye sura ya nne na mwisho kuna matokeo na mahitimisho ya utafiti. Suala muhimu linalojitokeza ni kuwa uhamisho hautokei tu kiholela bali hutawaliwa na kanuni mahsusi. Kwa jumla, utafiti huu umependekeza kuwa sintaksia ya uhamisho ifanywe katika lugha nyinginezo ili kuendeleza uwanja huu kwa nadharia za kisasa zaidi.

YALIYOMO


| Mada | Ukrasa |
|---|---|
| Anwani | i |
| Ikirari | ii |
| Tabaruku | iii |
| Shukrani | iv |
| Vifupisho | v |
| Maelezo ya Istilahi | vi |
| Ikisiri | viii |
| Yaliyomo | ix |
| **SURA YA KWANZA : UTANGULIZI** | 1 |
| 1.1 Suala la Utafiti | 5 |
| 1.2 Malengo ya Utafiti | 6 |
| 1.3 Maswali ya Utafiti | 6 |
| 1.4 Tahadhania | 6 |
| 1.5 Upeo wa Utafiti | 7 |
| 1.6 Misingi ya Kuchagua Mada ya Utafiti | 8 |
| 1.7 Tahakiki ya Maandishi | 9 |
| 1.7.1 Sintaksia na Uhamisho | 9 |
| 1.7.2 Maandishi Kuhusu Dhima | 10 |
| 1.7.3 Tafiti Bayana Kuhusu Uhamisho | 10 |
| 1.7.4 Maandishi Kuhusu Sarufi ya Lulogooli | 11 |




KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

1.8 Misingi ya Nadharia .. 12

1.9 Mbinu za Utafiti 20

1.9.1 Kusampulisha Data 21

1.9.2 Ukusanyaji wa Data 21

1.9.3 Uchanganuzi wa Data 22

1.9.4 Uwasilishi wa Data 22

**SURA YA PILI : VIGEZO VYA SENTENSI YA LULOGOOLI** 24

2.1 Majopo Leksia 24

2.1.1 Majopo Amilifu 33

2.2 Miundo Virai 36

2.2.1 Kirai Leksia 36

2.2.1.1 Kirai Nomino 36

2.2.1.2 Kirai Tenzi 39

2.2.1.3 Kirai Kivumishi 42

2.2.1.4 Kirai Kielezi 44

2.2.1.5 Kirai Kihusishi 45

2.2.2 Kirai Amilifu 46

2.2.2.1 Kirai Bainishi 46

2.2.2.2 Kirai Kipatanishi 47

2.2.2.3 Kirai Shamirishi 47

2.3 Muundo wa Sentensi 49

**SURA YA TATU: MUUNDO DHIMA** .............................................. 55

3.1 Kiarifu .............................................................................................. 55

3.2 Kiima ................................................................................................ 57

3.3. Shamirisho ........................................................................................ 58

**SURA YA NNE: UHAMISHO DHIMA** ................................................ 62

4.1 Uhamisho Dhima ................... ............................................................ 62

4.2 Kanuni Zinazotawala Uhamisho ........................................................ 68

4.2.1 Kanuni Hamishe ............................................................................. 68

4.2.2 Kanuni ya Ufungami ........................................................................ 69

4.2.3 Kanuni ya Uhamisho kwa Masafa Mafupi ....................................... 70

4.2.4 Kanuni Arifishi ................................................................................. 71

4.2.5 Kanuni Theta .................................................................................... 72

4.1.6 Kanuni ya Ulafi ................................................................................. 74

**SURA YA TANO: HITIMISHO**........................................ 77

5.1 Muhtasari wa Matokeo ..................................................................... 77

5.2 Mahitimisho ya Utafiti........................................................................ 80

5.3 Mapendekezo ya Utafiti..................................................................... 78

Marejeleo ................................................................................................. 82

Kiambatisho ............................................................................................. 84

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## Kitangulizi

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza vikwazo vya muundo na uhamisho wa dhima katika sentensi za Lulogooli kwa misingi ya Sintaksia Finyizi. Kwa mujibu wa Chomsky (1993, 1995) Sintaksia Finyizi ililenga kuondoa ugumu wa kuchanganua sentensi uliowekwa na nadharia ya Utawala na Ufungami kwa kutupilia mbali dhana ya muundo ndani wa sentensi na kufasiri upya nadharia za kanuni na vigezo. Isitoshe ilijaribu kurahisisha uwakilishi wa kinadharia kwa kuendeleza matumizi ya dhana chache za kuelezea sarufi. Mtazamo huu huzingatia hatua tatu muhimu ambazo ni hesabu ya maneno kupitia majopo ya kisarufi, muungano wa maumbo ili kuunda sentensi na uhamisho wa vijenzi katika kugeuza muundo wa sentensi. Hatua hizi zilihusishwa kwa ubayana zaidi na dhana ya dhima.

Dhima ni uhusiano wa kisintakisia baina ya virai nomino na kiarifu katika sentensi moja, zile zinazohusika huangaliwa kama kwamba zinajaliza kiarifu kwa namna ambavyo zinakuza matumizi ya kitenzi. Dhana ya dhima inategemea kwamba kiungo msingi cha sentensi yoyote ni kiarifu. Hivyo basi, huonekana kujengea maana ya kiarifu. Namna ambavyo neno hupewa dhima imefungamana na kanuni arifishi ambayo ni lazima muundo uafiki ili uwe mkamilifu. Kila kiarifu lazima kiwe na kiima. Kanuni hii ilitazamwa kulingana na uhamisho dhima.

Uhamisho wa dhima hautokei kiholela, umefungamana na kanuni kama vile utegemezi muundo na ufundani. Kanuni ya utegemezi muundo huhitaji kuwa uhamisho wowote umakinike na uzingatie mahusiano ya kisarufi ya vijenzi. Kanuni ya ufundani hueleza

kuwa kihamisho chochote hakitakiwi kusonga zaidi ya fundo mbili katika kielelezo tungo. Kanuni mbalimbali zilichanganuliwa, kulingana na matumizi yake katika sintaksia ya Lulogooli.

Kwa mujibu wa Frawley (2003), anayezingatia maoni ya wataalamu mbalimbali, Lulogooli ni lahaja mojawapo ya Kiluhya ambayo ni lugha ya Kibantu. Lugha za Kibantu hutegemea mfanano wa vikwazo vingi vya kisarufi katika nyanja za kifonolojia, kimofolojia na za kisintaksia. Kwa mfano, maneno yote yana silabi wazi, na pia yana muundo wa konsonanti na vokali. Tazama muundo wa maneno *guku* (nyanya) na *likele* (chura) yaliyowakilishwa hapo chini.

(1.1) Muundo wa maneno ya Lulogooli

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| g | u | k | u | | l | i | k | e | l | e |
| \| | \| | \| | \| | | \| | \| | \| | \| | \| | \| |
| K | V | K | V | | K | V | K | V | K | V |

Mojawapo wa vikwazo vya kimofolojia kuhusu mpangilio wa nomino katika ngeli ni kuzingatia mianzo ya hizo nomino, kwa mfano:

(1.2) Mifano ya ngeli za nomino

| **Ngeli** | **Neno (Umoja)** | **Neno (Wingi)** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| I – TSI | *imburi* (mbuzi) | *Tsimburi* (mbuzi) | mbuzi mbuzi |
| U – A | *umwana* (mtoto) | *avana* (watoto) | mtoto watoto |
| LI-MA | *litunda* (tunda) | *matunda* (Matunda) | tunda matunda |


Vile vile baadhi ya vigezo vya kisintaksia ni vile vya ngeli ya nomino kutawala muundo wa sentensi kwa njia ya upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano:

(1.3) Jedwali la upatanisho wa kisarufi

| **Ngeli** | **Neno (Umoja)** | **Neno (Wingi)** |
|---|---|---|
| I – TSI | *imburi **i**kuzi*<br>(mbuzi amekufa) | *Tsimburi **tsi**kuzi*<br>(mbuzi wamekufa) |
| U – A | *umwana **a**vuniki*<br>(mtoto amevunjika) | *avana **va**vuniki*<br>(watoto wamevunjika) |
| KI-VI | *Ekerenge **ki**vuniki*<br>(mguu **u**mevunjika) | *ivirenge **vi**vuniki*<br>(miguu **i**mevunjika) |
| UU-VU | *Uvwoni vukiri*<br>Dhambi imeenea | *Uvwoni vukiri*<br>Dhambi zimeenea |
| LI – MA | *Ligomia ligwi*<br>Ndizi limeanguka | *Magomia gagwi*<br>Mandizi yameanguka |

Upatanisho katika sentensi hizi ni tofauti kwa sababu ya ngeli tofauti za nomino. Nomino hizi huathiri viambishi awali kwenye kitenzi au fungu tenzi.

Lugha ya Lulogooli inazungumzwa katika eneo la magharibi mwa Kenya, Wilaya ya Vihiga (Taz. Ramani). Aidha maeneo mbalimbali ya wilaya hii pia huwa na lahaja tofauti. Utafiti huu utachunguza lahaja ya Lulogooli katika tarafa ya Vihiga, sehemu ya Buyonga, kwa sababu ndiyo lahaja ninayoelewa zaidi.



AREA = .......... . SQ. KILOMETRES
POPULATION ..................
IDAKHO
KAKAMEGA FOREST
BULUKHOSA
SHIRU
KISA
IDAKHO
CHAMAKANGA
BUGINA
BUMBO
KEGONDI
KISATIRU
NORTH
KEDOLI
CHAVAKALI
LUSENGELI
SHAMAKHOKHO
VIYALO
BUKULUNYA
MUDETE
GAVUDIA
NYANZA
EAST
MBALE
LYADUYWA
SENENDE
MARAGOLI
KIGAMA
SEREM
BUNYORE
BUGONDA
KIVAGALA
PROVINCE
KEGOYE
SOUTH
HAMISI NYANYORI
KAPSOTIK
MAGUI
GISAMBAI
HAMISI TILIKI
NYANGORI
LUGOVO
BUYONGA
MADZUU
BANJA
JEPKAYAI
IVORA
MARAGOLI
LEGEND
Provincial Boundaries
Location Boundaries
Sub-Location Boundaries
GIMARAKWA
TIGOI
MAHANGA
LUSIOLA
VIGULU
CHANGENDA
MASANA
GAMALENGA
0 1 2 3 4 5 MILES
NYANZA
PROVINCE

Sehemu hii inatudhihirishia misingi muhimu ya lahaja ya utafiti huu. Msukumo wa utafiti huu umejadiliwa kwa undani kwenye sehemu ya suala la utafiti.

## 1.1 Suala la Utafiti

Nadharia ya Sarufi Bia ilijaribu kuweka misingi ya kijumla kuhusu kanuni za lugha ya binadamu. Kila lugha ina vikwazo ambavyo hufuatwa katika matumizi. Utafiti huu ulichunguza vigezo na kanuni mbalimbali zinazotawala uhamisho dhima katika sentensi za Lulogooli. Uhamisho ni dhana muhimu katika sintaksia ya lugha yoyote ile kwa jumla. Kwa kadiri kubwa, dhana ya uhamisho inasaidia katika kuelewa kanuni na hali zinazotawala miundo mbalimbali ya sentensi kisarufi. Isitoshe mabadiliko ya miundo ya sentensi pia huchangia kutosheleza mahitaji ya sarufi na mawasiliano.

Sawa na lugha zingine, sintaksia ya Lulogooli inatumia aina mbalimbali za sentensi na kuna kanuni na hali za kimsingi zinazozitawala. Tafiti mbalimbali zimefanywa, lakini maandishi yaliyopo katika Kiswahili yanadhihirisha tafiti zilizofanywa katika uhamisho wa kichwa na kikanushi, virai nomino na viulizi (King'ori 2005; Kawa 2003; na Matu 1991). Katika lugha nyinginezo za Kiafrika, kuna utafiti wa kirai nomino katika Kiembu na Lubukusu (Nyaga 1998 na Wasike 1992). Hivyo basi hili ni dhihirisho kuwa uhamisho dhima, wala vigezo vingine vya muundo na uamilifu katika lugha nyingi hazijaangaliwa. Isitoshe jambo hili halijaelezwa katika sentensi za Lulogooli. Isitoshe ni kazi chache zinazoshughulikia lugha za Kiafrika zilizotumia nadharia ya Sintaksia Finyizi. Nyingi zilijifunga kwa nadharia ya awali ya Utawala na Ufungami. Pengo hili ndilo linalozua haja ya kueleza miundo hii na uhamisho dhima katika sentensi kwa kutumikiza nadharia ya kisasa yenye ushawishi thabiti. Kwa kujaribu kuangazia suala hili, utafiti huu uliazimia kuafiki malengo kadha wa kadha.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo manne bayana:

1. Kuchanganua sentensi ya Lulogooli kwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi ili kubainisha vigezo vyake kimuundo.
2. Kubainisha na kudhihirisha dhima katika sentensi sahili za Lulogooli.
3. Kueleza kanuni zinazotawala uhamisho dhima katika sentensi za Lulogooli.
4. Kutathmini utoshelevu wa Sintaksia Finyizi katika kueleza muundo na uhamisho dhima wa sentensi ya Lulogooli.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Malengo haya yalitazamiwa kujibu maswali yafuatayo;

1. Ni vigezo vipi mahsusi vinavyodhibiti sentensi sahili arifu ya Lulogooli kwa mujibu wa Sintaksia Finyizi?
2. Ni dhima zipi zinazodhihirika katika sentensi sahili za Lulogooli?
3. Ni kanuni zipi mahsusi zinazotawala uhamisho dhima wa sentensi za Lulogooli?
4. Sintaksia Finyizi inatosheleza kueleza uhamisho dhima katika sentensi za Lulogooli?

## 1.4 Tahadhania

Utafiti huu uliongozwa na tahadhania zifuatazo;

1. Sentensi sahili ya Lulogooli ina vigezo vya kimuundo ambavyo vinahusiana na dhima za kisintaksia
2. Uhamisho dhima wa sentensi za Lulogooli hutawaliwa na kanuni jumulifu za kisarufi.

## 1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti wa uhamisho katika sintaksia ulitazamiwa kueleza aina zote za uhamisho kwa kuzingatia muundo na uamilifu wa sentensi. Utafiti huu hauzingatii uhamisho wote bali umejikita tu katika uhamisho dhima wa sentensi za Lulogooli. Kazi hii, inajitosheleza kwa sababu uhamisho dhima hutawaliwa na kanuni tofauti na zile za uhamisho wa aina nyingine. Isitoshe miundo ya sentensi pia huweza kuelezwa kwa namna ya pekee kwa kuzingatia uhamisho wa dhima mbalimbali.

Kinadharia utafiti uliangazia uhamisho wa maumbo, ulichanganua dhima mbalimbali zinazoweza kuhamishwa na kuunda miundo tofauti ya sentensi kwa kuzingatia kanuni za uhamisho. Hivyo basi hatua mbili za muundo wa sentensi, ambazo ni idadishi ya maneno kupitia majopo ya kisarufi na muungano wa maumbo hazikuzingatiwa sana. Mambo haya yalituelekeza tu kwa namna ambavyo sentensi huundwa kwa misingi ya nadharia hii. Dhima zilizochunguzwa ni kiima na shamirisho kwa sababu kulingana na (Poole, 2002) ndizo zinazodhihirika wazi na pia hutokea kuathiri sintaksia zaidi. Dhima ya chagizo haikushughulikiwa kwa sababu hutumiwa kuelezea zaidi kiarifu. Isitoshe hatukushughulikia miundo ya dhima hizi kulingana na viarifu katika sentensi wala dhima ambazo hazitoi maana ya mtenda, mhisivu na mtendwa kwenye kiima na shamirisho, Kwani tutakuwa tumeingilia uwanja wa semantaki.

Sentensi zilizoshughulikiwa hapa ni sentensi sahili za Lulogooli kwa sababu muundo wake huweza kuonyesha mahusiano ya vijenzi kwa uwekevu zaidi kuliko sentensi zingine. Isitoshe umbo la sentensi sahili ni la kimsingi zaidi kuliko maumbo mengine. Sentensi changamano na ambatano hazikushughulikiwa kwa sababu sentensi hizi hutokana na sentensi ya kimsingi zaidi ambayo ni sahili.

## 1.6 Misingi ya Kuchagua Mada ya Utafiti

Tukitalii katika uwanja wa usomi tutatambua kwamba kazi nyingi zinazopatikana hulenga maswala ya kimofonolojia zaidi na sio ya kisintaksia. Isitoshe kazi nyingi za Lulogooli zinahusu sarufi kwa jumla pasipo kubobea katika maswala ya kinadharia. Kwa hivyo, Utafiti huu ulikusudiwa kupambanua na kuweka misingi zaidi katika sintaksia ya lugha za Kiafrika na Lulogooli kama lugha ya Kibantu.

Utafiti huu ulikusudia kuchangia kukuza sintaksia ya Lulogooli kwa kudhihirisha kanuni za uhamisho dhima kwa namna unavyoweza kuelezwa kwa misingi ya nadharia ya Sintaksia Finyizi.

Bali na mchango katika nadharia jumulifu, utafiti huu utawasaidia watafiti wanaonuia kufanya tafiti katika lugha za Kiafrika kupata msingi katika sintaksia, kanuni zinazotawala uhamisho dhima na athari zake kwa uchanganuzi wa kisemantiki . Jambo hili lilituonyesha moja kwa moja namna utafiti huu utakavyofaidi uwanja wa semantiki, kwani maana ya sentensi kisarufi hushughulikiwa na kitengo hiki cha semantiki. Yamkinika kuwa utafiti huu utakuwa muhimu pia katika uwanja wa pragmatiki kwa sababu uliweka msingi wa uchanganuzi wa mazungumzo: mazungumzo hudhihirisha miundo mbalimbali ya sentensi zenye uhamisho dhima. Utafiti huu utachangia katika ufundishaji wa lugha sio tu za Kiafrika hata Kiswahili. Kwani ni msingi bora wa kueleza mengi katika uwanja wa sintaksia kama vile majopo ya maneno, uundaji wa sentensi na kanuni zinazotawala uundaji huo.

Aidha utafiti huu utasaidia katika isimu linganishi, hasa pale ambapo sintaksia ya Lulogooli italinganishwa na nyingine yoyote ya Kiafrika hasa ya Kibantu kwa misingi

ya Sintaksia Finyizi. Hili litachangia katika kuchanganua na kueleza sarufi ya lugha za Kiafrika kama eneo la usomi. Sehemu hii imeangazia misingi ya uteuzi wa mada kwa kuzingatia umuhimu wa kinadharia na kimatumizi ya utafiti na namna ambavyo utakuza isimu kupitia sarufi ya lugha za Kiafrika. Tafiti za aina mbalimbali zilichangiana ilivyodhihirika katika sehemu ifuatayo ya mapitio ya maandishi.

## 1.7 Tahakiki ya Maandishi

Sehemu hii ya mapitio ya maandishi, iliangazia mambo muhimu yaliyoshughulikiwa kuhusu sintaksia na uhamisho kwa jumla na tafiti bayana ambazo zimewahi kufanywa kuhusu uhamisho.

### 1.7.1 Sintaksia ya Uhamisho

Waandishi wengi wameandika kuhusu sintaksia (Tazama: Chomsky 1981, 1986; Jacobson 1986; Radford 1988; 1997; Cook 1988; Cook na Newson 1996, na Habwe na Karanja 2002). Waandishi wameeleza baadhi ya mambo ambayo ni msingi katika sintaksia. Ingawa waandishi wengi wamejaribu kueleza dhana za sintaksia, dhana hizo zinaweza kuelezwa katika maeneo matatu makuu: vijenzi vya sarufi, miundo ya sintaksia na mageuzi katika sintaksia. Kwa mujibu wa waandishi hawa sintaksia hujihusisha na namna ambavyo maneno huunganishwa ili kuunda virai na sentensi kamili. Pia hushughulikia kanuni zinazotawala ufasiri kamili wa maneno hayo na virai. Vipengele vya kisintaksia hudhihirika katika miundo ya virai, kwa mfano kirai nomino, kirai tenzi, kirai kivumishi, kirai elezi, kirai husishi miongoni mwa virai vingine.

Sintaksia imekuwa na kupitia katika hatua mbalimbali, kutoka zile changamano hadi zile zinazozingatia kanuni wekevu zaidi. Kipengele hiki cha Sintaksia ndicho cha

kimsingi zaidi cha lugha na huunganisha kile cha kifonolojia na kileksia katika uundaji na mageuzi ya sentensi. Uhamisho wa vijenzi vile vile huchangia katika kueleza miundo mbalimbali ya sentensi, kwani hautokei tu bali huongozwa na kanuni mahsusi na hufuata utaratibu mwafaka.

### 1.7.2 Maandishi Kuhusu Dhima

Baadhi ya waandishi kama Habwe na Karanja (2002) na Radford (1988) wanaeleza na kutoa mifano kwa jumla ya kuonyesha dhima mbalimbali katika sentensi. Maelezo hayo yanachangia katika utafiti huu kwa sababu wanatudokezea jinsi dhima maana mbalimbali zinavyotokea katika sentensi. Wameeleza dhima maana kama vile mtenda, mtendwa, kifaa, mwathiriwa, nguvu, chanzo, lengo, wakati, mahali, matokeo na malighafi. Utafiti huu unashughulikia tu dhima za kiima au shamirisho zinazotoa maana ya mtenda, mtendwa na mhisivu. Radford (1997) ameeleza uhamisho wa dhima za mtenda, mtendwa na mhisivu. Maelezo yake ni msingi mzuri wa kazi hii kwani yametuwekea bayana baadhi ya kanuni bia zinazoongoza uhamisho na hatua zake.

### 1.7.3 Tafiti Bayana Kuhusu Uhamisho

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu uhamisho; miongoni mwazo ni kama vile; Nyaga (1980), Wasike (1992) na Kawa (2003) walifanya utafiti wa uhamisho wa Kirai Nomino. Nyaga (ibid), alishughulikia lugha ya Kiembu ambapo alieleza kwamba uhamisho wa Kirai Nomino hasa katika sentensi tendwa na kiambishi (wa) kiliongezwa kwa mzizi wa kitenzi kudhihirisha hali hii. Wasike (ibid) alieleza uhamisho huo katika sentensi sahihi za Lubukusu. Alionyesha kwamba uhusika ndio uliosababisha kuwepo kwa hali tendwa na uhamisho wa viulizi hauzingatii kanuni ya ufunge. Kawa (ibid) naye alizingatia sentensi za Kiswahili. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa uhamisho

ulisababishwa na utawala, ufungami, kanuni ya ufunge na utegemezi muundo. Tafiti hizi zilizingatia misingi ya nadharia ya Utawala na Ufungami. Baadhi ya kanuni walizotumia kueleza tafiti zao zilichangia katika kuelezea uhamisho dhima katika utafiti huu.

King'ori (2005) alishughulikia uhamisho wa kichwa na kikanushi katika sentensi za Kiswahili, kwa misingi ya nadharia ya Sintaksia Finyizi. Kazi yake ilitudhihirishia kwamba uhamisho hautokei kiholela na iwapo utatokea lazima kihamishe kisonge hatua chache hasa funge mbili. Pia uhamisho huo utategemea muundo wa sentensi. Jambo hili ni muhimu pia katika kueleza uhamisho wa dhima.

Tafiti hizi ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu zilitupa habari muhimu kuhusu vijenzi vya sentensi sahili katika lugha za Kibantu. Isitoshe zilitueleza baadhi ya kanuni ambazo hutumiwa au husababisha kuwepo kwa uhamisho. Lakini hazikugusia uhamisho wa dhima za kisintaksia katika sentensi za Lulogooli.

### 1.7.4 Maandishi Kuhusu Sarufi ya Lulogooli

Frawley (2003) alieleza kuwa lugha zinaweza kuoanishwa kwa kuzingatia sifa mbalimbali kama vile, miundo yao ya kifonetiki, kimofolojia, kimofonolojia na kisintaksia sababu za kinasaba miongoni mwa sifa nyinginezo. Lugha za Kibantu huwa na muundo wa sentensi ambao una kiima, kitenzi kisaidizi, kitenzi na kitendewa. Isitoshe, pia muundo wa kiima huathiri muundo wa maneno mengine yote yanayotumiwa katika sentensi. Mambo haya ni muhimu kwa sababu yalichangia kutupa vijenzi vya sentensi sahili za Lulogooli kama lugha mojawapo ya Kibantu.

Maandishi mengi yanayopatikana katika lugha ya Lulogooli yanazingatia fonolojia na sarufi. Hasa hulinganisha lahaja mbalimbali za Kiluhya au kutazama Kiluhya kwa jumla. Lidonde (1978) alishughulikia fonolojia zalishi katika lahaja ya Kiluhya ya Lwitakho Kasaya (1988) alitafiti juu ya hatua muhimu za kifonolojia katika lahaja za Lulogooli, Luwanga na Lubukusu.

Adagala (1979) alishughulikia namna maneno kama *Tsing* na *Tsya* ya Lulogooli yanavyotumiwa katika lugha na fasihi katika shule za msingi. Utafiti huu umejikita katika uwanja wa fonolojia, ingawa kuna baadhi ya sentensi zilizotudhihirishia vijenzi vya sentensi sahili za Lulogooli. Hivyo basi taarifa hii ni mwangaza wa kuendelea kutekeleza utafiti huu kwa sababu haujafanywa katika lugha ya Lulogooli.

Mapitio ya maandishi yalidhihirisha umuhimu wa dhana mbalimbali katika sintaksia, pamoja na pengo kubwa katika utafiti wa sintaksia ya Lulogooli. Hivyo basi kuna umuhimu wa kuchanganua namna uhamisho dhima unavyoweza kutokea na kuwasilisha kanuni zinazotawala uhamisho huo, kwa misingi ya kinadharia.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Nadharia tofauti zimetumiwa kuchanganua sintaksia. Sarufi Amilifu, kwa mfano, huzingatia mitazamo mipana miwili ambayo ni sarufi amilifu leksishi na sarufi amilifu mfumo. Mitazamo hii huhusishwa na kazi za Dik (1978, 1980) na Halliday (1974, 1994) yote ina uwiano kwa sababu inasisitiza uamilifu wa maana katika lugha. Hivyo basi nadharia hii haikutufaa katika utafiti huu kwani imeegemea sana katika matumizi ya lugha kimaana katika jamii wala sio maumbo ya matumizi: yaani husisitiza

semantiki zaidi kuliko sintaksia na tena haizingatia dhana ya uhamisho wa kisarufi. Nadharia mwafaka zaidi ni ya Sarufi Zalishi.

Nadharia ya Sarufi Zalishi iliyoendelezwa na Chomsky (1957, 1965, 1981, 1986, 1993 na 1995) ilidokeza hapo awali kuwa sintaksia ni mfumo wa sheria unaowakilisha ujuzi wa mtu binafsi kuhusu muundo wa sentensi. Malengo ya Chomsky yalikuwa kuweka misingi ya kanuni za kijumla za Sarufi Bia za lugha ya binadamu. Alisisitiza vigezo vya kisintaksia kama nanga muhimu ya sarufi (Taz. Cook na Newson, 1996). Nadharia hii ilipitia hatua mbalimbali kwa mfano ilibainisha dhana za umilisi na utendaji wa lugha pamoja na kutenganisha miundo ya sentensi: muundo ndani na muundo nje. Bali na haya mtazamo huu ulibainisha aina mbili za sheria sintaksia; sheria msingi na sheria mageuzi. Katika sheria msingi ndimo mifumo ya leksia hubainika. Haya yaliendelezwa zaidi na kuelezwa katika Sintaksia Zalishi pambanuzi.

Chomsky (1981, 1986) alifafanua kanuni bia na vigezo vinavyohitajika kuendeleza Sarufi Bia ya isimu zalishi. Nadharia ya kanuni na vigezo si moja ila hujumuisha vijinadharia sita ambavyo hujengana na kutegemeana ambavyo ni X-Baa, utawala, uhusika, dhima maana, ufungami na ufundani.

- X - Baa : Nadharia jumulifu ya muundo kirai
- Utawala : Uhusiano wa kichwa cha kirai na shamirishi zake
- Uhusika : Amali ya pronomino au nomino kulingana na hadhi ya kiima au yambwa ya kiarifu.
- Dhima maana: Uhusiano wa kisemantiki baina ya virai nomino na kiarifu.

- Ufungami : Uhusiano wa baina ya pronomino, anafora na visabiki vyao.
- Ufundani : Kanuni ambayo huzingatia kikwazo cha uhamisho wa maumbo kutoka pahala fulani kwenda pengine.

Utaratibu wa uchanganuzi wa kisintaksia kwa kuzingatia vijinadharia hivi ulikuwa changamano sana. Chomsky (1995) alirahisisha utaratibu husika kwa kuzindua Sarufi Finyizi. Ili kupunguza uchangamano huo alizingatia hatua mbili muhimu:

(i) Kutupilia mbali dhana ya muundo ndani wa sentensi

(ii) Kufasiri upya nadharia za Utawala na Ufungami na kuziwakilisha; kama Kanuni za Vigezo vya Sarufi Bia sahili zaidi.

Sintaksia Finyizi kama Sarufi Bia inaendeleza imani kuwa sintaksia ni kitengo msingi zaidi cha muundo wa kisarufi. Katika kuangalia sentensi, Sintaksia Finyizi inatambua hatua tatu muhimu:

(i) Idadishi ya maneno kupitia majopo ya kisarufi.


(ii) Muungano wa maumbo ili kuunda sentensi sanifu

(iii) Uhamisho wa maumbo katika kugeuza muundo wa sentensi

Majopo ya maneno hurejelea zile aina pana za maneno zinazobainishwa kupitia matumizi ya kisarufi. Dhana hii hujifunga kwenye vitengo viwili; cha kileksia na kiamilifu (majopo muundo). Majopo yanayopambanuliwa kupitia sifa za kileksia ni matano; Nomino (N), Vivumishi (V), Vitenzi (T), Vihusishi (H), Vielezi (E). Majopo muundo yanayounganisha maneno yote na yanayotambulikana wazi zaidi ni matatu:

vibainishi (B), Viunganishi (U) na Vishamirishi (SH). Kwa mfano kauli kama *Umwana umrahi yingii yengo* 'Mtoto mzuri ameingia nyumbani' ina idadisha ifuatavyo:


(1. 4) Upambanuzi wa majopo ya maneno leksia




Ubainishi wa majopo ya maneno unaashiria hatua ya kwanza ya kuunda na pia kufasiri sentensi kwa namna fulani akilini. Utambuzi kama huu utaingiliana moja kwa moja na taratibu za kuunganisha majopo ya maneno ndiyo kuunda virai na tungo ndefu zaidi. Taratibu hizi na kanuni zake zinaangaliwa katika hatua ya muungano.


Muungano ni mapatanisho ya majopo ya maneno ili kuunda virai na pia kuambatanisha virai sahili ili kuunda virai jumlifu zaidi hadi sentensi kamili kujengeka. Kwa mfano sentensi kama vile *Umwana uyu akina vurahi* 'Mtoto huyu anacheza vizuri' inajumuisha virai viwili yaani *Umwana uyu* 'mtoto huyu' na *akina vurahi* 'anacheza vizuri'. Sentensi hii huundwa kwanza kwa kuunganisha *Umwana* 'mtoto' na *Uyu* 'huyu' yaani anaunganisha nomino na kivumishi ili kuunda kirai nomino (KN). Katika mchoro matawi itakuwa:

(1.5) Muungano katika Kirai Nomino




Kisha *akina* 'anacheza' huungana na *vurahi* 'vizuri' kuunda kirai tenzi (KT).

(1.6) Muungano katika Kirai Tenzi




Hiki kirai nomino na kirai tenzi huungana ili kuunda kirai jumlifu zaidi au sentensi sahili. Kulingana na sarufi salishi, sentensi sahili hutazamwa sawa na kishazi. Kwa minajili ya uwiano wa kinadharia, kishazi huwakilishwa sawa na kirai patanishi (KP). Zingatia kielelezo kifuatacho.

(1.7) Muungano katika Kirai Patanishi




Virai huungana ili kuunda sentensi kamili kwani, haiundwi tu mara moja. Hatua ambazo hutumika katika uchanganuzi ndizo huaminika hutumika kuziunda akilini na msikilizaji huzitumia kufasiri. Utaratibu kama huu unaonyesha muundo wa sentensi

katika lugha inayoangaliwa pamoja na kanuni zinazotawala muundo huo. Kanuni za jumla zinazojitokeza ni kama vile:

(i) Utegemezi muundo

(ii) Ufungami

(iii) Ufasili kamili

(iv) Kanuni leksia

Kanuni ya Utegemezi Muundo huzingatia kwamba muundo mahsusi wa kisarufi hutokea tu katika hali mahsusi ya kisarufi (Radford 1997). Yaani hali yoyote ya kisarufi hutegemea muundo. Sentensi huundwa kutokana na majopo mahsusi ya maneno. Kila neno katika sentensi lina ujopo kisarufi kwa mfano:

(1.8). Jedwali la ujopo wa maneno

*Avakana yava vayanza vimuli*

Wasichana hawa wanapenda maua

Nomino kivumishi kitenzi nomino

Kanuni ya Ufungami hueleza uhusiano baina ya pronomino, anafora na virejeleo vyao. Hivyo basi, ufungami hurejelea zaidi viwakilishi kwa jumla kwa namna ambavyo vina uhusiano na maneno mengine katika muktadha wa sentensi. Sintaksia hii hubainisha maneno ya aina tatu; rejeleo, pronomino na anafora. Kwa mfano:

(1.9) *Mama yakwira*

Mama amejikata

Sentensi hii inabainisha kisabiki na anafora. Kisabiki kimewasilishwa na neno mama yaani umbo hili si lazima lirejelee maana nyingine katika sentensi bali kitu kilicho nje ya sentensi moja kwa moja; Umbo kama *kwi* 'ji' katika *yakwikara* 'amejikata' ni mfano wa anafora. Ina maana kuwa umbo mahsusi inarejelea kitu ambacho tayari kimetajwa katika sentensi. Pronomino sio lazima ifungwe na kisabiki. Kwa mfano:

(1.10) *Umwana yamletela oyo*

Mtoto alimletea yeye

*Oyo* 'yeye' ni pronomino.

Ufungami hasa husisitiza anafora na kisabiki. Kila wakati anafora inahitaji kufungwa hivyo basi huzingatia kanuni ya Ufungami. Kanuni ya ufasili kamili hushikilia kuwa kila kipengele cha sentensi yoyote kimepewa maana kutegemea kiwango chake mahsusi kwa mfano umbo leksia lazima liwe na dhana zote za kisemantiki ambazo zitadhihirisha dhana za kiisimu za kauli fulani na umbo fonetiki pia lazima liwe na dhana za kifonetiki zinazodhihirisha utamkaji. Kanuni ya Leksia hushikilia kwamba muundo wa sentensi hutegemea maneno leksia yanaoiunda. Hivyo basi leksia ya maneno lazima izingatiwe katika sintaksia.

Kanuni hizi ni sifa bia ambazo hutokea katika lugha yoyote ile. Ilivyodokezwa hapo awali. Mojawapo wa kanuni bayana ambayo hujitokeza katika lugha ya Lulogooli ni upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi huzingatia kwamba viambishi mwanzoni mwa vitenzi katika sentensi huathiriwa na ngeli ya nomino husika.

Upatanisho huo hutofautiana kutoka ngeli moja hadi nyingine. Hizi ndizo kanuni muhimu zinatawala muungano wa majopo ya maneno katika lugha ya Lulogooli.

Vijenzi vinavyoundwa huweza kuhamishwa kutoka pahala fulani na kupelekwa pengine kwa madhumuni bayana ya kisarufi. Uhamisho huu hutekelezwa kwa namna rudifu. Baadhi ya waandishi kama Radford (1997) na Poole (2002) wanaeleza uhamisho wa aina mbalimbali ukiwemo uhamisho dhima huku wakizingatia Sintaksia Finyizi na Utawala na Ufungami. Uchanganuzi wao unatudhihirishia kwamba kuna kanuni na hali maalum zinazosababisha uhamisho. Uhamisho husababisha kuwepo kwa aina mbalimbali za sentensi kimuundo kila unapotokea.


Kulingana na kanuni arifishi kila kiarifu cha kiwango cha juu lazima kiwe na kiima, jambo ambalo husababisha kuwepo kwa uhamisho wa vijenzi kutoka pahala pa awali hadi pengine. Baada ya uhamisho nafasi ya kihamishe ndiyo hubaki. Hali hii hutawaliwa na kanuni ya kategoria tupu. Kwa mfano:.

(1.11) *Umwana uyu akina vurahi*

Mtoto huyu anacheza vizuri

Baada ta uhamisho, kimchoro matawi itakuwa:

(1.12)



Bali na hizi hatua tatu kuu za Sintaksia Finyizi baadhi ya vikwazo vitakavyozingatiwa ni kwamba:

(i) Uhamisho hutekelezwa tu pale ambapo unakubalika wakati na mahala ambapo panafaa.

(ii) Uhamisho pale ambapo kihamisho huafiki na hujitosheleza kimofonolojia.

(iii) Uhamisho hutelekezwa tu kwa kuzingatia hatua chache

Vikwazo hivi hulingana na kanuni tatu za uhamisho wa kisintakisia: ucheleweshi, ulafi na masafa mafupi kwa mujibu wa sintaksia finyizi. Kwa ujumla utafiti uliendelezwa kwa misingi ya nadharia ya Sintaksia Finyizi kwa sababu hutudhihirishia kwa uwekevu zaidi namna ambavyo uhamisho wa dhima unavyoweza kutokea. Sehemu inayofuata inaeleza mbinu zilizotumiwa kufanya, kuchanganua na kuwasilisha data ya utafiti.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Kule maktabani vitabu mbalimbali vinavyoeleza dhana muhimu zinachochangia ufanisi wa utafiti huu vilisomwa. Mazungumzo katika hali halisi yalisikilizwa miongoni mwa watu tofautitofauti na sentensi zenye sifa mahsusi kuchaguliwa kwa minajili ya kueleza utafiti huu. Data ilihusisha sentensi za Lulogooli zilizoshirikisha dhima. Sentensi zilichaguliwa kwa misingi kuwa ni sahili. Mbinu za utafiti zilijumuisha hatua nne muhimu ambazo ni:-

(i) Kusampulisha data

(ii) Kukusanya data

(iii) Kuchanganua data

(iv) Kuwasilisha data

### 1.9.1 Kusampulisha Data

Mbinu ya kusampuli data iliyotumiwa ni ile ya kusampuli kwa lengo maalum. Sentensi ambazo zinathibitisha kanuni na dhima zinazohitajika zilitumiwa. Mbinu nyinginezo za kusampuli kama vile kusampuli kwa kupanga watu katika makundi mbalimbali. Kusampuli kwa njia sahili ambapo vitu vinavyosampuliwa hupewa nambari pasipo kuzingatia utaratibu fulani maalum, hatukuzingtia kwa sababu sentensi lazima ziwe ni sahili na pia zidhihirishe dhima mbalimbali kwa uwekevu zaidi. Vile vile kusampuli kwa kuchukua sampuli baada ya hatua kadhaa zilizoamuliwa hukukufaa. Kwani huenda tungepata data ambayo haingetimizia bayana zaidi malengo ya utafiti huu.

### 1.9.2 Kukusanya Data

Data ilihusisha sentensi tofautitofauti sahili za Lulogooli zilizochaguliwa kutoka kwenye vitabu vya Lulogooli na mazungumzo mahsusi. Data ilikuwa na sentensi sahili ambazo ni arifu, yakinishi za katika kauli tenda. Vitabu vifuatavyo vilitumiwa kupata data;

(i) Lugadiru, J. *et al* (1968): *Afandi na Kaana Keke;* TKK Supplimentary Reader 1: Lulogooli, Nairobi, Longman.

(ii) Gachukia, E. W. *et al* (1968): *Isindu ne Ingida Yeye;* TKK Supplimentary Reader 2: Lulogooli, Nairobi, Longman.

(iii) Lugadiru, J. *et al* (1970): *Engoko Yagoota;* TKK Supplimentary Reader 1: Lulogooli, Nairobi, Longman

(iv) Lugadiru, J. *et al* (1971): *Lisoosa Lyokutwekitsa Muhiga;* TKK Supplimentary Reader 3: Lulogooli, Nairobi, Longman.

Vitabu hivi viliteuliwa kwa sababu vina sentensi sahili za Lulogooli ambazo zinafaa kwa utafiti huu. Katika kukusanya sentensi hizi nilisoma vitabu hivi, nikasikiliza na hata kunasa kwenye kinasa sauti mazungumzo ya kawaida ya watu katika jamii. Sentensi zilitafsiriwa kwa Kiswahili.

Idadi ya sentensi zilizotumiwa ni kumi na tisa; sentensi hizi zilidhihirisha dhima mbalimbali zinazoweza kueleza kwa wazi zaidi, kanuni zinazotawala uhamisho dhima. Hili lilifikiwa kwa kufanya majaribio ya uhamisho wa dhima hizo kwa kuzingatia kanuni zinazohitajika. Haya yote yalielezwa katika hatua ya uchanganuzi wa data.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi ulianza kwa uainishaji wa sentensi kulingana na dhima zilizodhihirisha. Dhima zilizoshughulikiwa ni kiima na shamirisho. Kanuni hizi zilihusisha kutazama majopo ya maneno, taratibu za kuunga kwa maneno ili kuunda sentensi na namna ambavyo uhamisho dhima huathiri miundo ya sentensi.

### 1.9.4 Uwasilishaji wa Data

Data iliwasilishwa kwa kueleza muundo wa sentensi kwa kutazama namna majopo ya maneno yanavyoungana. Maelezo ya kanuni zilizotawala uhamisho, uhamisho dhima, mifano na vielelezo matawi vilitumiwa ili kudhihirisha kila sentensi. Dhima zilizohamishwa zilionyeshwa kwa kutumia athari zilizoachwa kwa kutumia michoro matawi. Sentensi mbalimbali zilitumiwa kuonyesha miundo iliyoundwa baada ya uhamisho.

KENYATTA UNIVERSITY

**Hitimisho**

Tumetalii masuala muhimu yaliyojenga msingi wa utafiti huu. Upeo na mipaka, nadharia ya utafiti na mbinu za kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data miongoni mwa masuala mengine yameelezwa. Baadhi ya maswala muhimu yaliyojitokeza ni kwamba utafiti wa sentensi sahili za Luloogoli na hata lugha nyinginezo za Kiafrika hazijashughulikiwa pakubwa kwa misingi ya nadharia hii ya Sintaksia Finyizi. Isitoshe kuna utaratibu na kanuni maalum zinazotawala ujenzi wa sentensi. Miundo ya sentensi sahili za Lulogooli imeelezwa kwa msingi muhimu katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# VIGEZO VYA SENTENSI YA LULOGOOLI

**Kitangulizi**

Katika sura ya kwanza, tuliona kwamba Sintaksia Zalishi inalenga kufasili kanuni Jumulifu zinazotawala muundo wa sentensi. Kwa mujibu wa Radford (1997), sentensi ni muungano wa virai unaozingatia vigezo vya kisarufi. Muundo wa virai nao hutegemea majopo ya maneno. Sura hii kwa hivyo itadhihirisha vigezo vya sentensi ya Lulogooli kupitia awamu tatu za uchanganuzi sintaksia, majopo ya maneno, miundo virai na uamilifu wa sentensi.

## 2.1 Majopo ya Maneno

Majopo ya maneno ni kategoria za maneno ambazo zina sifa za kisarufi zinazofanana. Upatanisho na unyambuaji wa mofolojia ya maneno ni dhihirisho mwafaka la kutenga majopo ya maneno. Kisintaksia kila jopo huchukua nafasi fulani maalum katika sentensi. Majopo ya maneno kisarufi yanaweza kuanishwa kwa makundi mawili makuu:

(i) Jopo la kileksia

(ii) Jopo la kiuamilifu.

### 2.1.1 Majopo Leksia

Leksia ni dhana ya kisarufi ambayo huhusika na mizizi ya maneno. Kila neno la kileksia limeingizwa katika Kamusi; huhusisha sifa za neno kisintaksia, maana utumikaji na namna ambavyo huungana na maneno mengine kileksia na hata virai.

Vitengo vya kileksia vinaweza kujadiliwa kwa mtazamo wa kimofoloja na sifa za kisintaksia. Dhana za kileksia zinaweza kuainishwa kama majina kwa sababu zina sifa za kimofolojia ambazo zinafanana aidha kwa kuzingatia umoja na wingi wao au namna ambavyo huunda maneno mengine. Majopo Leksia ni matano: nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, na vihusishi.

Nomino ni maneno yanayotumiwa kutajia watu, vitu, mahali na hali mbalimbali. Kuna njia mbalimbali za kutambulisha nomino, ambazo ni: Semantiki; huzingatia maana ya majina, Mofolojia; huzingatia viambishi vya mwanzo vya nomino na Sintaksia; hushughulikia hasa upatanisho wa kisarufi wa vitenzi sentensi.

Kwa kuzingatia uainishaji wa kisemantiki kuna aina sita kuu za nomino zilizowakilishwa katika jedwali lifuatalo:

(2.1) Jedwali la aina za nomino

| Nomino | Kigezo | Jina | Maana |
|---|---|---|---|
| Dhahania | Majina yanayotaja vitu vya kufikirika | Uvurwaye<br>Uvuyanzi<br>Ovovereri | Ugonjwa<br>Furaha<br>Huzuni |
| Nomino za pekee | Majina maalum ya watu au mahali | Anguzuzu<br>Omido<br>Kisumu<br>Ikumba | |
| Nomino za jamii | Hutaja watu, vitu au mahali kwa jumla | Kivara<br>Avandu<br>Avasomi<br>Tsimesa | Dunia<br>Watu<br>Wanafunzi<br>Meza |
| Nomino za wingi | Hutumiwa kutaja vitu visiovyohesabika | Amatsi<br>Amavere<br>Umyeke | Maji<br>Maziwa<br>Mchanga |
| Nomino za jamii | Hutaja watu au vitu kwa makundi | Ikiduma cha avandu | Halaiki ya watu |
| Kitenzi Nomino | Nomino hutokana na vitenzi kutumiwa mahala pa nomino | Kwiga<br>Kuzia<br>kukina | Kujifunza<br>Kwenda<br>kucheza |

Mpangilio wa kimofolojia huzingatia viambishi awali vya nomino maneno katika umoja na wingi. Hizi ni ngeli za nomino, ambazo huweza kulinganishwa na zile za lugha za kibantu kwa jumla.

(2.2) Jedwali la mifano ya ngeli za nomino:

| Ngeli | Mifano<br>Jina | Maana |
|---|---|---|
| U - A | *Umwana* | mtoto |
| | *Avana* | watoto |
| I – TSI | *Inyumba* | nyumba |
| | *Tsinyumba* | nyumba |
| LI – MA | *Ligomia* | ndizi |
| | *Magomia* | ndizi |
| E – TSI | *Endeve* | kiti |
| | *Ttsindeve* | viti |
| E – I | *Ekeverenge* | mguu |
| | *Ivirenge* | miguu |
| LU – TSI | *Lugaga* | ua |
| | *Tsingaga* | maua |
| U – U | *Uvuyanzi* | furaha |
| | *Uvuyanzi* | furaha |

Kwa msingi wa sintaksia nomino huainishwa kulingana na namna inavyooana na vitenzi vinavyotumiwa katika sentensi moja kwa umoja na wingi.

(2.3) Jedwali la upatanisho wa kisarufi

| Ngeli | Mifano ya Upatanisho | Visawe kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| U - VA | Umwana **a**kina<br><br>Avana **va**kina | Mtoto anacheza<br><br>Watoto wanacheza |
| I – TSI | Imbuli **i**kuzi<br><br>Tsimbuli **tsi**kuzi | Mbuzi amekuja<br><br>Mbuzi wamekufa |
| KI – VI | Ekerenge **ki**vuniki<br><br>Ivirenge **vi**vuniki | Kiti kimevunjika<br><br>Viti vimevunjika |
| VU – VU | Uvurwaye **vu**kiri<br><br>Uvurwaye **vu**kiri | Ugonjwa umezidi<br><br>Ugonjwa umezidi |
| LI-GA | Litunda **li**gwa<br><br>Matunda **ga**gwi | Tunda limeanguka<br><br>Matunda yameanguka |
| LU-TSI | Lugaga **Lu**gwi<br><br>Tsinganga **tsi**gwi | Ua limeanguka<br><br>Maua yameanguka |

Jedwali hili pia linadhihirisha upatanisho wa kisarufi ambapo aina ya nomino ndiyo hutawala muundo wa sentensi.

Kijopo kingine leksia ni vitenzi ambavyo ni maneno yanayodhihirisha vitendo. Kuna aina mbalimbali za vitenzi kama vile: Vitenzi vikuu ni maneno ambayo hubeba maana kuu ya kitendo na hayana viambishi.

(2.4) *kina* 'cheza', *yimba* 'imba', *sira* 'vuka' *sara* 'omba'

Vitenzi visaidizi hutumiwa pamoja na vitenzi vikuu ili kuleta maana inayokusudiwa katika sentensi kama vile:

(2.5) *yari* 'kuwa', *yanza* 'penda'

Vitenzi halisi navyo huwa na viambishi awali vya nafsi na njeo kwa mfano:

(2.6) Ninaenda, ninacheza, ninaruka.

Vitenzi vinginevyo ni kama vile vitenzi vishirikishi vipungufu, vitenzi vishirikishi vikamilifu na vitenzi sambamba. Vitenzi navyo hutambulishwa na viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi yao isiyobadilika. Kwa mfano:

(2.7) (a) *deka* (pika)

(b) *kina* (cheza)

Kitenzi katika (a) kina mzizi 'dek' na (b) 'kin'

Dhana za kisarufi kama vile nafsi, wakati, idadi na mnyambuliko hutambulishwa na aidha viambishi awali au viambishi tamati mwafaka vilivyoambishwa kwenye mizizi ya vitenzi. Kwa mfano:

(2.8) *Yadeka* *(ya + deka)*

(Alipika) (ali + pika)

Katika mfano huu, kiambishi awali 'ya' – kinasimamia nafsi ya tatu katika umoja na wakati uliopita.

(2.9) *Dekerwa* - *dek + e + rwa*

(pikiwa) - pik + i + wa)

Katika mfano huu, kiambishi tamati *-erwa* kimeongezwa kwenye mzizi wa kitenzi. Kiambishi hiki hubadilisha muundo na maana ya kitenzi asilia *dekerwa* – inamaanisha kuwa kiima alifanyiwa kitendo cha kupikiwa.

Vitenzi huelezwa zaidi na vielezi. Bali na vitenzi, hufafanua vivumishi na vielezi vingine. Kuna aina mbalimbali za vielezi;

(2.10) Jedwali la aina za vielezi

| AINA YA VIELEZI | MAELEZO | MIFANO VIELEZI | MAANA |
|---|---|---|---|
| Vielezi vya namna | Hueleza jinsi au namna ambavyo jambo hufanyika | Garaha garaha<br>Vwangu vwangu | Pole pole<br>Haraka haraka |
| Mahali | Sehemu tendo lilitendeka | Mkiguti<br>Yengo<br>Kisumu | Uwanjani<br>Nyumbani<br>Kisumu |
| Wakati | Muda wa kutendeka kwa jambo | Hamgorova<br>Mmavweve<br>kale | Jioni<br>Machweo<br>Kale/zamani |
| Idadi | Tendo limetendeka mara ngapi. Hawa aidha maalum au isiyoweza kuhesabika (jumla) | Hali kavaga<br>Kumaliza<br>Hali kanyingi | Mara tatu<br>Mwisho<br>Mara nyingi |

Mfano mwingine wa jopo leksia ni vivumishi. Haya ni maneno yanayoelezea zaidi kuhusu nomino. Kuna aina mbalimbali za vivumishi kama vile:

Vivumishi vya sifa huelezea sifa za nomino kwa mfano:

(2.11) *-rahi* '-zuri'; *-kivi* '-baya'; *vyera* 'bora' n.k.

'*Umwana umrahi*' (mtoto mzuri).

Vivumishi vya Idadi huelezea idadi ya nomino kwa mfano:

(2.12) *vingi* 'wengi', *vadi* 'wachache'

*Avana vanne* 'watoto wanne'

Vivumishi viashiria ni vivumishi vinavyoonyesha mahali ambapo nomino ipo. Yaweza kuwa karibu, mali kidogo au mbali zaidi na mzungumzaji kama vile:

(2.13) *yaha* 'hapa', *yaho* 'hapo' *hara* 'pale'

*Umwana uyu* 'mtoto huyu'

*Umwana oyo* 'mtoto huyo'

*Umwana ura* 'mtoto yule'

Vivumishi viashiria vya kuthibitisha hutumiwa kusisitiza umbali wa nomino husika kutoka kwa mzungumzaji kama vile:

(2.14) *Yaha yaha* 'papa hapa', *yaho yaho* 'papo hapo', *hara hara* 'pale pale'

Vihusishi pia ni mojawapo wa jopo leksia ambalo huonyesha uhusiano uliopo kati ya vitu viwili, kama vile:

(2.15) *Shimbi na* 'karibu na'

*Ihare na* 'mbali na'

*Harovega ha* 'kando ya'

Bali na umoja na wingi. Kuna sifa za uundaji wa maneno ambazo hutusaidia kuainisha maneno kileksia. Ili kuunda maneno mengine, maneno asilia huongeza mofimu aidha mwanzo au mwisho wa hilo neno. Vitenzi kwa mfano vinaweza kuongezwa mofimu mahususi ili kuunda majina, kulingana na mifano ifuatayo;

(2.16) Uundaji majina kutoka vitenzi

| **Vitenzi** | | **Nomino** |
|---|---|---|
| *Kuza* | - | *likuza* |
| (kufa) | - | (kifo) |

| | | |
|---|---|---|
| *Kunika* | - | *kikuniko* |
| (funika) | - | (funiko) |
| *Yigitsa* | - | *umwigitsi* |
| (funza) | - | (mwalimu) |
| *saala* | - | *lisaala* |
| (omba) | - | (ombi) |

Majina pia yanaweza kuundwa kutoka kwa majina mengine:

(2.17) Uundaji wa majina

| **Majina** | - | **Majina** |
|---|---|---|
| *Umwigitsi* | - | *Uvwigitsi* |
| (Mwalimu) | - | (Ualimu) |
| Lisaala | - | Umsaali |
| (Ombi) | - | (Muombaji) |

Vitenzi na majina ndio hudhihirisha sifa hizi kwa uwekevu na kwa wingi sana kimatumizi. Majina hutambulishwa kwa namna ambavyo wingi wao hutokana na idadi husika, hivyo basi huwa na umoja na wingi mahsusi.

Aina mbalimbali za majopo ya maneno yanaweza kutumiwa pahala fulani maalum katika kirai au sentensi. Maneno mbalimbali katika jopo la majina yanaweza kutumiwa katika sehemu moja. Zingatia sentensi:

(2.18) *Avana vasira umgoye (endeve, umpira, umsara)*

(Watoto wanaruka kamba (kiti, mpira, mti)

Jina *umgoye* 'kamba' linaweza kubadilishana pahala na maneno mengine katika jopo hili kama vile *endeve* 'kiti', *umpira* 'mpira' au *umsara* 'mti' tukichukulia kuwa dhana ya maana sio muhimu hapa.

Kitenzi pia kinaweza kubadilishana pahala na vitenzi vingine katika virai au sentensi, kwa mfano:

*(2.19) Guku adeka (akina, aritsa, yiimba)*

Nyanya anapika (anacheza, anakula, anaimba)

Maneno ya kileksia ambayo yanaweza kuainishwa kama vivumishi pia hubadilishana pahala kwa mfano:

*(2.20) Amaua yaga na marahi (ammbi, maravu, amamwamu)*

Maua haya ni mazuri (mabaya, meupe, meusi)

Vielezi na vihusishi pia hubadilishana pahala. Mifano iliyojadiliwa inaonyesha kuwa bali na vipengele vya kimofolojia, vile vya kisintaksia pia vinaweza kutumiwa kudhihirisha aina ya maneno kileksia. Ikiwa neno litatumiwa kubadilishana pahala na neno kutoka jopo lingine kileksia basi sentensi itakayoundwa haitakuwa sanifu. Kwa mfano:

*(2.21)* (a) *Guku adeka*

(Nyanya anapika)

(b) *Guku umgoye* (v)

(Nyanya kamba)

(c) *Guku halovega* (H)

(Nyanya kando ya)

Sarufi ya Lulogooli itazingatia matumizi ya maneno kileksia kwani hii ni hatua moja muhimu katika uundaji wa sentensi. Mjadala huu wa dhana za mofosintaskia za kutazama maneno leksia ni muhimu kwetu kutambua namna ambavyo maneno haya huungana ili kuunda sentensi sahihi kisarufi. Sehemu inayofuata tutajadili majopo ya maneno kiuamilifu.

### 2.1.2 Majopo Amilifu

Majopo haya yana umuhimu wa kumatinisha maana leksia bali hayawakilisha maana ya kimsingi. Majopo ya kiuamilifu yanayotambulikana wazi zaidi ni matatu: Vibainishi, Viunganishi, Vishamirishi.

Vibainishi ni maneno kama viwakilishi, vimikilishi na viashiria. Vibainishi hutumiwa badala ya au kueleza mahala ambapo nomino husika ipo. Maneno haya yanaweza kutumiwa kabla au baada ya nomino. Kwa mfano:

(2.22) Endeve *yiyi* yakuvunika

Kiti **hiki** kimevunjika

Viwakilishi ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Kuna viwakilishi vya aina mbalimbali kama vile: Viwakilishi vya nafsi huru, nafsi tegemezi, vimilikishi, vya idadi vya ngeli, vya 'a' unganifu, vya sifa miongoni mwa viwakilishi vingine.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

(2.23) Jedwali la mifano ya viwakilishi

| (a) Nafsi Idadi | Kiima<br>Nafsi huru | Yambwa<br>Nafsi tegemezi | Miliki |
|---|---|---|---|
| Umoja | Nzi (Mimi) | Nzi (ni) | -ange (-angu) |
| Wingi | Kunyi (Sisi) | Ku (tu) | -itu (-etu) |
| Umoja | Yivi (wewe) | U (U) | -icho (-ako) |
| Wingi | Munyi (nyinyi) | M (M) | -inyu (-enu) |
| Umoja | Oyo (yeye) | a (a) | -icheke (ake) |
| Wingi | Yavo (wao) | va (wa) | -avo (-ao) |

Viashiria ni kitengo cha maneno ambacho hutumiwa kuonyesha umbali wa vitu kutoka kwa anayezungumza. Vitu vinaweza kuwa karibu na, mbali kidogo na mbali zaidi ya anayezungumza.Zingatia jedwali:

(2.24) Jedwali la mifano ya viashiria

| Karibu na<br>Umoja Wingi | Mbali kidogo<br>Umoja Wingi | Mbali zaidi<br>Umoja Wingi |
|---|---|---|
| Uyu (huyu) – yava (hawa)<br>Yiki (hiki) – yivi (hivi)<br>Yiyi (hii) – yizi (hizi)<br>Yigu (huu) – yiji (hii) | Uyo(huyo) – yavo (hao)<br>Yicho (hicho)-yivyo (hivyo)<br>Yeyo (hiyo) – yizyo (hizo)<br>yigwo (huo) – yijo (hiyo) | Ura (yule) – Vara (wale)<br>Kira (kile – vira (vile)<br>Yira (ile) – zira (zile)<br>Ura (ule) – Jira (ile) |

Viambishi vingine hujitokeza kama viambishi vilivyoambishwa kwenye vitenzi. Huwa ni viambishi vya ngeli vinavyotudhihirishia idadi ya nomino husika na wakati. Kwa mfano:

*(2.25) Vyakogota* - *vya-ko-gota*

Vimepotea - vi-me-potea.

*Vya* ni kiambishi cha upatanisho wa ngeli ya (Ki – Vi) na *-ko-* ni kiambishi kinachoonyesha wakati timilifu.

Viunganishi navyo hutumiwa kuunganisha maneno au virai ili kuunda sentensi moja iliyokamilika. Maneno kama *kandi* 'tena', *navuzwa* 'lakini', *ne* 'na', *handi* 'labda' na *kigira* 'kwa sababu'. Kwa mfano:

*(2.26) Yazia navuzwa kwamgaya*

(Alienda lakini tulimkataza)

Katika huo mfano *navuzwa* 'lakini' limetumiwa kama kiunganishi cha virai viwili. *Yazia* 'alienda' na *kwamgaya* 'tulimkataza'.

Shamirisho ni maneno ambayo hutumiwa kutanguliza kishazi katika sentensi ndefu zaidi. Shamirisho ni muhimu kwa sababu hututambulisha ikiwa sentensi ni kauli arifu au swalifu. Maneno kama vile: *niva* 'ikiwa', *hee* 'na' na *ndi* 'yote' kwa maana ya kwamba. Kwa mfano:

*(2.27) Nayanze niva nahevwe umdoga*

(Atafurahi ikiwa atapewa gari)

Neno *Niva* 'ikiwa' limetumiwa kama shamirishi katika sentensi hiyo huonyesha kwamba sehemu wanayotanguliza ni kishazi. Sehemu hii imejadili kuhusu majopo leksia na majopo ya uamilifu. Majopo haya ni muhimu sana katika uundaji wa virai ambavyo ndivyo msingi wa uundaji wa sentensi.

### 2.2.0 Miundo Virai

Virai ni vifungu vya maneno ambavyo ni sehemu ya sentensi, huwa ni vipashio vya kimuundo vyenye zaidi ya neno moja. Kuna aina mbili kuu za virai:

(i) Kirai leksia

(ii) Kirai amilifu

### 2.2.1 Kirai Leksia

Maneno leksia ndiyo maneno tawala katika kirai hiki. Kuna virai leksia vitano ambavyo ni: Kirai nomino, Kirai kitenzi, Kirai kivumishi, Kirai kielezi, Kirai kihusishi.

#### 2.2.1.1 Kirai Nomino

Nomino ndilo neno tawala katika kirai nomino, aghalabu ndilo neno ambalo hutangulia kuna miundo mbalimbali ya kirai nomino.

(a) Nomino pekee inaweza kuunda kirai kwa mfano:

(2.28) *Umwigitsi yazi*

Mwalimu amekuja


*Avasomi vakina*

Wanafunzi wanacheza

KN → N

N → Mwigitsi

(2.29)




Nomino mbili zinaweza kuunda kirai, kwa mfano:

(2.30) (a) *Guga na guku varima*

Babu na nyanya wanalima

(b) *Eng'ombe ni imburi tsiritsa*


Ng'ombe na mbuzi wanakula

KN → $N_1 + N_2$

$N_1$ → Guga

$N_2$ → Guku

(2.31)



(c) Nomino na kivumishi vile vile huweza kuunda kirai nomino.

(2.32) (a) *Umsara umnene gugwi*

Mti mkubwa umeanguka

(b) *Endeve nguzuzu ivuniki*


Kiti kidogo kimevunjika

KN → N + V

N → Umsara

V → umnene

(2.33)




(a) Namna nyingine ya kuunda kirai nomino ni kwa kutumia nomino ya kirai tenzi.

(2.34) (a) *Umwigitsi aziza*

Mwalimu anaenda

(b) *Misara jigwi jiromba makaradasi*


Mti iliyoanguka hutengeneza makaratasi

KN → N + KT

N → Umwigitsi

KT → aziza

(2.35)




#### 2.2.1.2 Kirai Tenzi

Neno tawala katika hiki ni kitenzi. Kuna miundo mbalimbali kwa mfano

Kitenzi kimoja kinawaza kuunda kirai tenzi.

(2.36) (a) *Kogeriza*

Tunajaribu

(b) *Vaviti*

Wamepita

KT → T

T → Kogeriza

(2.37) (a) *Vakina umpira*

Wanacheza mpira

(b) *Yamuha amapopo*

Alimpa paipai


Kitenzi na nomino moja. Pia hujitokeza kama muundo wa kirai tenzi.

KT → T + N

T → vakina

N → umpira

(2.38)




Kirai tenzi hujitokeza kama kitenzi na nomino mbili

(2.39) (a) *Vamha umsomi ikaramu*

Walimpa mwanafunzi kalamu

(b) *Vavatuma amaduma mwiduka*

Waliwatuma mahindi dukani


KT $\longrightarrow$ T + $N_1$ + $N_2$

T $\longrightarrow$ Vamha

$N_1$ $\longrightarrow$ Umsomi

$N_2$ $\longrightarrow$ ikaramu

(2.40)



Kitenzi na kitenzi vilevile huunda kirai tenzi.


(2.41) (a) *Ayanza kuria*

Anapenda kula

(b) *Vamkonya kuginga*

Walimsaidia kubeba

(2.42)




(e) Kitenzi, nomino na kitenzi

(2.43) (i) *Kwenya avana vaze*

Tunataka watoto waje

(ii) *Leka tsing'ombe tsaye*

Wacha ng'ombe wale


KT ⟶ T + N+ T

T ⟶ kwenya

N ⟶ avana

T ⟶ vaze

(2.44)




**2.2.1.2 Kirai Kivumishi**

Virai hivi huongozwa na kivumishi. Vile vile kuna miundo tofauti,

Kivumishi na kielezi chake kwa mfano

(2.45)

(a) *-rahi mno*


-zuri kabisa

KV ⟶ V + E

V ⟶ -rahi

E ⟶ mno

(2.46)



(b) - *komeru mno*

- nono sana

Kivumishi na nomino hujitokeza kama kirai kivumishi.

(2.47) (a) - *ene midoga*

- enye magari

(b) - *ene mulimi*


- enye shamba

KV → V + N

V → - *ene*

N → *midoga*

(2.48)




(c) Kivumishi na kirai tenzi vile vile huunda kirai kivumishi

(2.49) (a) - *ene akina vurahi*

- enye kucheza vizuri

(b) - *ene kuginga misigo minyingi*


- enye kubeba mizigo mingi

KV → V + KT

V → - ene

KT → akina vurahi

(2.50)




**2.2.1.4 Kirai Kielezi**

Ni fungu la maneno ambalo hueleza jinsi kitu kilivyofanyika, mahali kilipofanyika au wakati kwa mfano:

(2.51) (a) *Mno mno*

Sana sana


(b) *Mmavwevwe kuzya yengo*

Asubuhi na mapema tulienda nyumbani

(c) *Mgamba*

Kesho

(2.52)



### 2.2.1.5 Kirai Kihusishi

Kirai kihusishi hutumia maneno kama *wa* 'kwa' *na* 'na' *harovega hi* 'kando ya' (m – (katika) Yakifuatwa na nomino au kikundi nomino, kwa mfano:

(2.53) (a) *Msikulu mwavo*

Katika shule yao

(b) *Harovega hi nzira*

Kando ya barabara


Aghalabu kirai kihusishi hutangulia nomino, Kama vile:

KH $\longrightarrow$ H + N

H $\longrightarrow$ Harovega hi

N $\longrightarrow$ inzira

(2.54)




Virai hivi vilivyojadiliwa ndivyo virai leksia kwa namna ambavyo huundwa kutokana na maneno leksia. Hili huangazia maana msingi ya sentensi yoyote ile ambayo huamilishwa na virai amilifu.

### 2.2.2 Virai Amilifu

Virai hivi ni vikubwa zaidi kwa kuunganisha neno tawala na virai vingine au majopo mengine ya maneno leksia. Virai hivi hutawaliwa na maneno kutoka kwenye jopo amilifu ambavyo ni: Virai vibainishi, vipatanishi na shamirishi.

#### 2.2.2.1 Virai Vibainishi

Viwakilishi au viashiria vikitumiwa katika kifungu huunda kirai kibainishi kwa mfano:

(2.55)

(a) *Umwana ura yaza*

Mtoto yule anakuja

(b) *Yengo wavo ni hare*

Nyumbani kwao ni mbali


KB ⟶ N + B + T

N ⟶ Umwana


B ⟶ Ura

T ⟶ Yaza

(2.56)



(2.57)




**2.2.2.2. Virai Vipatanishi**

Kipatanishi kikitumiwa kutanguliza sentensi huunda kirai patanishi. Hujitokeza kama viambishi vya nafsi na wakati vinavyoambishwa kwenye vitenzi.

Kirai patanishi pia kinaweza kuungana na kirai tenzi. Kingine ili kuunda kirai tenzi kikubwa zaidi ambapo kirai tenzi ndicho shamirisho la kitenzi kwa mfano:

(2.58) *(a) Arazia*

Ataenda

KP ⟶ P + T

PA ⟶ ara

T ⟶ zia

**2.2.2.2 Virai Shamirishi**

Maneno tawala katika virai shamirishi ni kama *niva* 'ikiwa' na *ndi* 'kwamba' kwa mfano:

(2.59) (a) *Ndi yazya yengo*

Kwamba alienda nyumbani

(b) *Niva avana vayanza uvukinu*


Ikiwa watoto wanapenda mchezo

KSH → SH + KT

SH → ndi

KT → yazya yengo

(2.60)




Kirai shamirishi ni kikubwa kuliko virai vingine. Kirai hiki hundwa pia kwa kuunganisha shamirishi na kirai patanishi. Kwa mfano:

(c) *Niva vayanza*

Ikiwa wanapenda

KSH → SH + KP


SH → niva

KP → P + T

P → va

T → yanza

(2.61)




Sehemu hii imeshughulikia namna ambavyo virai mbalimbali huundwa. Muundo wa virai ndiyo msingi wa uundaji muundo wa sentensi zenye maana. Hili ni dhihirisho kuwa sentensi hazitokei tu kiholela bali hufuata utaratibu fulani.

## 2.3 Muundo wa Sentensi

Kwa mujibu wa sintaksia virai, maneno ya lugha hujiunga kuunda virai vyenye maana ya kisarufi ambavyo hujiunga kuunda sentensi. Sentensi ni neno au fungu la maneno linalopasha habari kamili. Kama lugha nyingine za kibantu, sentensi za Lulogooli huchukua muundo wa kirai nomino na kirai tenzi kwa mfano:

(2.62) (a) *Umwana akina amagina*

Mtoto anacheza mawe

S ⟶ KN + KT

KN ⟶ N

N ⟶ Umwana


KT ⟶ T + N

T ⟶ akina

N ⟶ amagina

Huweza kuwakilishwa ifuatavyo:

(2.63)




(b) *Umsara umtambi gugwi vwangu*

Mti mrefu ulianguka haraka

S ⟶ KN + KT

KN ⟶ N + V


N ⟶ Umsara

V ⟶ Umtambi

T ⟶ gugwi

E ⟶ vwangu

(2.64)





Sentensi ya neno moja huwakilisha nafsi, wakati na kitenzi, Kwa mfano:

(2.65) (i) Avanyagura → A + va + nyagura

Atakimbia → A + ta + kimbia

Nafsi wakati kitenzi

(2.66)




Vile vile virai leksia na virai amilifu hufumana ili kuunda kirai kikubwa zaidi ambacho ndicho sentensi kwa mfano:

(2.67) (a) *Umwana anyagura*


Mtoto anakimbia

KP → KN + KT

KN → umwana

KT → anyagura

(2.68)



(b) *Kuzaa mgamba*


Tutakuja kesho

KP ⟶ KT + KE

KT ⟶ kuzaa

KE ⟶ mgamba

(2.69)




Kwenye muundo huu wa sentensi. Sehemu ya kirai nomino huamilisho kiima na kirai tenzi huamilisha kiarifu shamirisho chagizo. Kwa mfano:

(2.70) (a) Baba yaiza tsing'ombe

Baba anachunga ng'ombe

Kiima kiarifu shamirisho

(b) Baba yaiza tsing'ombe virahi

Baba anachunga ng'ombe vizuri


Kiima kiarifu shamirisho chagizo

Sentensi za Lulogooli huongozwa na kanuni bia ambazo ni kanuni leksia na utegemezi muundo pamoja na kanuni mahsusi ambayo ni upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi ni dhana ambapo ngeli ya nomino huathiri kiambishi awali cha kitenzi katika sentensi husika.

Miundo ya sentensi hutegemea aina ya majopo ya maneno yaliyotumiwa hasa kiima na kiarifu (Cook na Newson 1996). Hili limedhihirika pia katika sentensi za Lulogooli. Kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (2.71) | (a) | *Umkana umrahi yakuza* | *Avakana varahi vakuza* |
| | | Msichana mzuri amekuja | wasichana wazuri wamekuja |
| | (b) | *Endeve indahi ivuniki* | *Tsindeve tsindahi tsivuniki* |
| | | Kiti kizuri kimevunjika | Viti vizuri vemevunjika |

(2.72)




Katika sentensi hizi kima huathiri kiambishi awali cha kivumishi na kitenzi. Viambishi 'U' na 'YA' katika mfano wa kwanza hukubaliana na maneno yanayopatikana katika ngeli ya 'U – VA'. Tofauti na mfano wa pili ambapo upatanisho wa kisarufi 'I-TSI' huwa katika ngeli ya 'E – TSI'.

Majopo leksia hushirikiana na majopo amilifu ili kuunda sentensi zenye miundo mbalimbali. Sentensi hizi ni muhimu kwani ndizo hujitokeza katika matumizi ya lugha ya Lulogooli.

**Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia muundo wa sentensi za Lulogooli kwa jumla. Imedhihirisha kuwa sentensi ina vijenzi ambavyo huainishwa katika majopo mahsusi ya kisarufi. Majopo haya ni Jopo Leksia na Jopo Amilifu.

Jopo Leksia lina nomino jina, kitenzi, vihusishi, vielezi na vivumishi na Jopo amilifu lina vibainishi, vipatanishi na shamirishi. Ili kupata sentensi sahih lazima majopo haya yabainishwe kisha yaunganishwe. Huunganishwa kwenye hatua ya pili ya idadishi ya majopo. Haya hutokea kwa kuzingatia kanuni mwafaka. Kanuni bia ni kanuni leksia na utegemezi muundo. Lakini ile mahsusi ni upatanisho wa kisarufi. Uamilifu katika sentensi huelezwa kupitia dhana kama vile kiima, kiarifu na shamirisho. Sentensi yoyote, ili iwe kamilifu kimaana sharti iwe na kiima ambacho huwakilishwa na nomino, na kiarifu ambacho ndicho hubeba ujumbe katika sentensi. Vijopo vingine vya maneno kisarufi huteuliwa kwa kuzingatia maana zao kileksia ai kiamilifu.

Sura hii imetuelezea bayana dhana muhimu za vijenzi na muundo wa sentensi za Lulogooli. Huu ni msingi wa kutubainishia dhima za kisintaksia katika sentensi.

# SURA YA TATU

# DHIMA KATIKA LULOGOOLI

## 3.0 Kitangulizi

Kwa kuzingatia Radord (1997) anaeleza kuwa dhima ni msamiati uliokopwa na wanaisimu kutoka kwa filosofia. Hueleza umuhimu wa dhana fulani katika maumbo ya sintaksia katika sentensi. Kwa mfano

(3.1) *Juma amkuyi Yohana*

Juma alimchapa Yohana

Sentensi hii ni kirai ambacho kina kiarifu *amkuyi* 'alimchapa na dhima zake mbili, Juma na Yohana. Hizi dhima mbili zinaamilisha wahusika katika kitendo cha *kuya* 'chapa' ambapo moja ni kiima na nyingine ni shamirisho. Maelezo ya (Palmer, 1994) yanashikilia kuwa Shamirisho huwa ndani ya mfungo wa kiarifu na kiima huwa nje, hivyo basi, shamirisho huitwa pia dhima ya ndani ilhali kiima huitwa dhima ya nje. Umbo la dhima ya kiarifu huamilisha maelezo ya dhima zinazohusishwa na kiarifu na nafasi zao.

## 3.1 Kiarifu

Katika sura ya pili tuliona kuwa nanga ya ujumbe katika sentensi ni kiarifu: kiarifu pia ndicho humiliki dhima katika sentensi. Kwa mfano:

(3.2) *Umwana akungi imbwa*

(Mtoto alifukuza mbwa)

*Umwana* ni kiima na *akungi imbwa* ni kiarifu.


Kiarifu huwa na dhima moja au zaidi. Katika mfano wa awali *akungi* 'alifukuza' ni kiarifu na kuna dhima mbili *umwana* 'mtoto' na *imbwa* 'mbwa'. Kiarifu humilikia uhusiano uliopo kati ya dhima hizi (mtoto na mbwa). Hivyo basi muundo wa sentensi hii ni:

Dhima ——— Kiarifu ——— dhima

KN ——— KT ——— KN

Kimchoro matawi itakuwa:

(3.3)




Muundo huu wa kiarifu hutokea katika lugha zote (Ta. Palmer 1994) na dhima hutofautiana katika uhusiano wa kisintaksia na kiarifu. Pia hubainishwa kupitia kwa athari zao kisarufi.

Hivyo basi katika baadhi ya sentensi dhima hubainishwa kupitia kwa muundo wa sentensi. Ikiwa dhima mbili zitabadilishana pahala basi muundo wao kisintaksia utabadilika. Kwa mfano:

(3.4) *Imbwa ikunga umwana*

(Mbwa anafukuza mtoto)

Basi 'mbwa' ndiye aliyesababisha kitendo cha kufukuza mtoto. Uwakilishi wa muundo dhima, kama:

(3.5) *Kunga (imbwa, umwana)*

Fukuza (mbwa, mtoto)

Waandishi mbalimbali wamejaribu kueleza dhana hii ya dhima ya maneno kisarufi katika sentensi. Katika sintaksia itakuwa aidha kiima au shamirisho.

Jukumu la dhima katika sentensi huamilishwa na kiarifu. Kuna baadhi ya viarifu ambavyo huhitaji dhima mbili au tatu ilhali vingine huhitaji tu dhima moja. Jambo hili hutokea kwa kuzingatia maana ya kiarifu, (Taz. Poole 2002), kwa mfano:

(3.6)1.1.1.1. (a) *Umwana agona*

(Mtoto analala)

(b) *Umwana akubi likele*


(Mtoto alipiga chura)

Kutokana na 3.5 (a) na (b) tunaona kuwa kiarifu 'agona' (analala) kina dhima moja ya kiima *umwana* 'mtoto' na kiarifu *akubi* 'alipiga' ina dhima ya kiima na shamirisho yaani *Umwana* 'mtoto' na *likele* 'chura'

## 3.2 Kiima

Hii ni sehemu mojawapo muhimu ya kirai. Aina ndogo zaidi ya kirai kinachoweza kuundwa hutokana na kiima na kiarifu ambapo aghalabu kiarifu huwa ni kitenzi. Kwa mfano, katika kirai *Juma akina* 'Juma anacheza', kiima ni Juma na kiarifu ni kitenzi *akina* 'anacheza'.

(3.7)




Kiima katika kirai ni kile ambacho hufanya kitendo kinachowakilishwa na kitenzi. Vile vile, kiima cha kirai ni sehemu ambayo hupatikana na kutambulisha ngeli, nafsi na njeo. Kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| (3.8) | *Arazya* | (ataenda) |
| | *Varazya* | (wataenda) |

Kiambishi *a* huwakilisha ngeli ya A – VA katika umoja; *ra* 'ta' huwakilisha wakati ujao. Katika sentensi kiima huamilisha dhima nje. Swala la namna ambavyo kiima hupewa theta ni tatu. Marantz (1984) na Chomsky (1986) hueleza kwamba kiarifu huvipa theta dhima za ndani (shamirisho) kwa namna iliyo wazi. Lakini kiima hakitegemei tu kiarifu bali hutegemea kiarifu na shamirisho.

### 3.3 Shamirisho

Hiki ni kipengele cha uamilifu wa sentensi. Huwa ni sehemu ya sentensi inayoonyesha kinachoathiriwa na nomino na huja baada ya kiarifu. Kinaweza kuwa kitendwa au kitendewa. Kuna aina tatu za shamirisho:

(a) Kipozi

(b) Kitondo

(c) Ala au kitumizi


Shamirisho kipozi ni jina la mtu au kitu kinachopokea athari za kitenzi. Pia huitwa yambwa au mtendwa. Kwa mfano:

(3.9) *Guga avoha eng'ombe*

Babu anafunga ng'ombe

*Eng'ombe* 'ng'ombe' ni shamirisho kipozi.

(3.10)





Shamirisho kitondo ni jina la kitu au mtu wa tatu anayepokezwa athari za kitenzi kupitia kwa kipozi. Huitwa yambiwa au mtendewa. Kwa mfano:

(3.11) (a) *Guku yadekera guga ovosera*

Nyanya alimpikia babu uji

*Guga* 'babu' ni shamirisho kitondo

(3.12)





(b) *Umwigizi azii ku mdoga*

Mwalimu ameenda kwa gari

*Ku mdoga* 'kwa gari' ni shamirisho ala.

Shamirisho hujulikana kama dhima ndani kwani huathiriwa kwa njia iliyo wazi na kiarifu.

(3.13)



**Hitimisho**

Sura hii imeangazia namna ambavyo dhima zinavyojitokeza katika Lulogooli. Ni dhahiri kwamba kiarifu ndio msingi muhimu unaotambulisha aina za dhima katika sentensi. Kuna baadhi ya viarifu ambavyo huchukua tu dhima moja na vingine ambavyo huwa na dhimba mbili ili ziweze kutoa maana kamili. Sehemu inayofuata inaeleza utaratibu na kanuni zinazotawala uhamisho wa hizi dhima.

# SURA YA NNE

# UHAMISHO DHIMA

**Kitangulizi**

Uhamisho wa dhima ni suala lililoweza kuepuka katika sintaksia ya lugha yeyote ile. Hii ni njia muhimu ya kueleza miundo mbalimbali ya sentensi inayoweza kutokana na utaratibu wa uhamisho. Vile vile, hueleza mbona baadhi ya sentensi ni sahihi na wala sio zingine. Hivyo basi tutaeleza namna ambavyo uhamisho wa dhima za kiima na shamirisho hutokea katika Lulogooli.

## 4.1 Taratibu za Uhamisho Dhima

Tuligundua hapo awali kuwa kiarifu huamilisha theta kiima, hivyo basi uchaguzi wa kiima hutegemea kiarifu kilichotumiwa katika sentensi. Jambo lingine ni kuwa uamilishi theta wa muundo wa sentensi huongozwa na kanuni bia ambayo hushikilia kuwa kila dhima hubeba jukumu theta tu na kila theta moja hupewa tu dhima moja tu. Kwa mfano:

(4.1) *Tsing'ombe tsilitsa maduma mumulimi*

Ng'ombe wanakula mahindi shambani


*Tsing'ombe* 'ng'ombe' hupewa dhima ya kiima, ilhali *maduma* 'mahindi' hupewa dhima ya shamirisho.

Sentensi hii ikibadilishwa katika kauli tendwa dhima hizo zitabakia tu vivyo hivyo. Kwani ng'ombe ndiye anayetekeleza kitendo cha kula mahindi; na mahindi ndiyo yanayoathiriwa na kitendo hicho.

Kitenzi ndicho msingi wa sentensi yoyote ile, hivyo basi huwa msingi katika muundo wowote ule wa sentensi. *Tsing'ombe* 'ng'ombe' hujitokeza kwanza kama kiima cha shamirisho *Maduma mumulimi* 'mahindi shambani' kisha husonga juu kwa hatua rudilifu na kuwa kiima cha kitenzi *lista* 'kula' kabla ya kusongezwa hatua moja zaidi. Juu ya kubainisha *tsi* 'wa'.

Katika mchoro matawi hiyo sentensi itawakilishwa ifuatavyo;

(4.2)



Tukichukulia kuwa vibainishi au shamirisho haviamilishi theta maana bali ni kitenzi pekee, basi dhima ya *Tsing'ombe* 'ng'ombe' ni kiima. Tunaweza kuchukulia kuwa *tsing'ombe* ilisonga hatua nyingine kuwa kiima cha *tsi* 'wa' kwa sababu ya upatanisho wa kisarufi. Ililazimishwa kusonga kwa namna rudilifu ili kutosheleza kanuni ya kusonga hatua chache.


Mfano mwingine katika kauli tendwa ambapo ni tokeo la uhamisho wa shamirisho kutoka pahala pa awali hadi pale pa kitambuzi, kiima cha kiarifu kwa mfano:

(4.3)1. *Uvayanze avana vadi*

Uwapende watoto wadogo


Watoto wadogo hubeba dhima ya shamirisho kwa sababu kitendo cha kupenda kinamwathiri. Katika mchoro matawi itakuwa:

(4.4)




Dhima ya shamirisho ikihamishwa itachukua muundo ufuatao:

(4.5)





Sentensi kama hii inadhihirisha kuwa kitenzi penda hubeba dhima mbili, hapa ambapo dhima moja pekee imetumiwa inaashiria kwamba sentensi hii haijakamilika, au labda ingeendelezwa katika kauli tendwa.

(4.6) Vayanzwi avana vadi

Wapendwe watoto wadogo

(4.7)




Wakati mwingine dhima ya kiima huweza kuwakishwa na vibainishi vya idadi kwa mfano:

(4.4) *Vosi vakina mukiguti*

(Wote wanacheza uwanjani)


Katika sentensi hii *vosi* 'wote' inaamilisha dhima ya kiima. Dhana hii ya vibainishi vya idadi vikidhihirishwa muundo wa sentensi hii ni;

(4.9)




*vosi* 'wote' ikisonga kwa hatua rudilifu huwa na muundo huu:

(4.10)




Tukichukulia kuwa kanuni bia huafikisha muundo wa dhima na muundo wa sintaksia kwa namna ambavyo hufanana, basi huonekana kuwa dhima mbili hutosheleza majukumu sawa kuzingatia kiarifu fulani kilichotumiwa. Haya huelezwa katika nadharia ya uamilishi sawa wa dhima iliyoelezwa kwa undani na Baker (1988) na ambayo husema kwamba viarifu tofauti huamilisha kutegemea nafasi yake kisintaksia. Hili linadhihirisha kwamba kiima katika kauli tendwa kwa mfano:

*(4.11) Avasomi vagumirwi*

Wanafunzi walishikwa

Kiima tendwa *avasomi* 'wanafunzi' ina dhima ya shamirisho ya kiarifa *gumira* 'shika'. Hivyo basi *avasomi* 'wanafunzi' hutoka kama shamirisho ya kitenzi *gumirwa* 'shikwa'. Ikiwa ni hivyo ilitokeaje kuwa *avasomi* 'wanafunzi' wakawa kiima cha kibainishi 'va' (wali-)? Hii ni kwa sababu kiima *avasomi* 'wanafunzi' husongezwa juu. Kwa hatua rudifu kwanza kuwa kiima cha kauli tendwa *gumirwa* 'shikwa' kisha kiima cha kibainishi *va* 'wali'.

(4.12)



Hivyo basi *avasomi* 'wanafunzi' hutokea kama shamirisho, ambapo hubadilika katika kauli tendwa yaani kutoka kwa shamirisho ya *gumirwi* 'shikwa' hadi kiima chake, kisha husongezwa juu kuwa kiima cha kibainishi.

Uhamisho tulioshughulikia unatuonyesha wazi kwamba huongozwa na kanuni mbalimbali mahsusi. Isitoshe kiarifu mbalimbali huamilisha dhima kiima na shamirisho zake kwa njia mbalimbali.

## 4.2 Kanuni Zinazotawala Uhamisho

Jukumu kuu la nadharia yoyote ni kueleza taratibu za kanuni zinazoitawala muundo na uamilifu wao katika sentensi na sintaksia ya uhamisho dhima. Kuna kanuni bia zinazojitokeza kwani Uhamisho uliodhihirika katika mifano ya hapo awali haukutokea tu kiholela bali uliongozwa na kanuni zifuatazo.

(i) Kanuni hamishe

(ii) Kanuni ya ufungami

(iii) Kanuni ya uhamisho kwa masafa mafupi

(iv) Kanuni ya kiarifu

(v) Kanuni theta

(vi) Kanuni ya ulafi


### 4.2.1 Kanuni Hamishe

Kanuni hii hushikilia kwamba kila uhamisho wa dhima utekelezwe kutoka pahala pa chini hadi juu. Pia huhitaji kuwa kila kinachohamishwa kiwache hamishe ambayo imefundwa na kitawala chake, kulingana na kanuni ya ufungami. Kwa mfano:

(4.13) *Imali yanyagura yengo vwangu*

Imali alikimbia nyumbani haraka

(4.14)




Baada ya uhamisho nomino hamisho Imali itasonga kutoka mahala pa chini hadi juu huku ikiacha hamishe tupu ambayo imefundwa na pronomino zake.

Uhamisho kutoka mahala pa chini hadi juu hutekelezwa kwa sababu kanuni hii huchukulia kuwa pahala pa kirai panaweza kuundwa tu kwa muungano na kichwa bali sio uhamisho ilhali pahala pa kiima panaweza kuundwa kwa muungano au uhamisho.

### 4.2.2 Kanuni ya Ufungami

Kanuni hii huhitaji kuwa muundo wa kijenzi kilichofundwa uamuliwe na neno tawala linalofaa. Hushikilia kuwa kifundo kama vile anafora au kihamishe lazima iathiriwe kimuundo na pronomino zao. (Taz. 4.1). Tukirejelea mfano huo;

*Tsing'ombe tsilitsa maduma mumulimi*

Ng'ombe wanakula mahindi shambani

Katika huu mfano, kiima cha kihamishe *maduma* 'mahindi' huamuliwa na kufundwa na kihamishe cha kiima cha kitenzi *litsa* 'kula' na mwishowe huamuliwa na kufundwa na *tsing'ombe* ambalo ni kiima cha kibainishi *tsili* 'wana'

(4.15) Tsing'ombe tsili $_{ha}$ tsa $_{ha}$ maduma mumulimi



### 4.2.3 Kanuni ya Uhamisho kwa Masafa Mafupi

Kanuni hii huhitaji kuwa dhima ihamishwe kwa nafasi ya kiima ya juu inayofaa kwa muundo husika. Vile vile uhamisho huu unaweza kuhusishwa na kazi ya Rothstein (1995) ya kanuni ya kiarifa ambapo viarifa huhitajika kuwa na kiima. Dhana hizi mbili husababisha kuwepo kwa uhamisho kwa namna rudilifu. Kwa mfano:

*(4.16) (a) Umwigitsi yatsia musikulu*

Mwalimu alikuja shuleni

Baada ya uhamisho hiyo sentensi itakuwa:

(b) *Umwigitsi ya (ha) tsia (ha) musikulu*

Mwalimu a $_{(na)}$ likuja $_{(na)}$ shuleni



Kwanza mwalimu ilikuwa kiima cha *musikulu* ambapo ilihamishwa na kuwa kiima cha kitenzi *tsia* 'likuja' kisha mwishowe ikahama na kuwa kiima cha kibainishi *ya-* 'a'. Hizo ndizo hatua chache ambazo kiima *umwigitsi* Mwalimu ingesonga kwa namna rudilifu.

### 4.2.4 Kanuni Arifishi

Kanuni hii hushikilia kwamba kila kiarifu lazima kiwe na kiima. Jinsi tulivyotambua hapo awali kwamba neno msingi katika sentensi ni kiarifu kwa sababu ndio hubeba ujumbe. Aghalabu kiarifu huwa ni kitenzi, hivyo basi sharti kuwepo na kile kinachopokea athari ya kitendo kinachowasilishwa. Kwa mfano:

(4.17) *Mama yatsa yengo*


Mama alikuja nyumbani

Kiarifu ni *tsa* '-kuja' Kimchoro matawi ni:

*-tsa mama yengo*


Kuja mama nyumbani

(4.18)




Hivyo basi lazima pawepo na kiima yaani:

(4.19)




### 4.2.5 Kanuni Theta

Hii ni kanuni ya sarufi Bia ambayo hushikilia kwamba kila dhima hubeba theta moja tu na kila theta moja huamilisha dhima moja tu. Kanuni hii ni muhimu katika sintaksia ya uhamisho na hata ile tendwa. Hivyo basi shamirisho ya kitenzi tendwa yaweza kuandikwa na kuelezwa katika kauli tendwa lakini sio shamirisho ya kitenzi tenda.

(4.20) (a) *Eng'ombe yakwivwa*


Ng'ombe imeibwa

(b) *Eng'ombe kwiva*

Ng'ombe iba..

Katika sentensi ya (i) ng'ombe ni kiima cha sentensi tendwa katika (ii) ng'ombe haiwezi kuwa kiima ya kauli tenda. Lakini itachukua nafasi hiyo tu baada ya uhamisho.

(4.21)




Kiarifu *kwiva* katika kauli ya kutenda huhitaji dhima mbili. Yaani kiima na shamirisho. Hivyo basi kiarifu *kwiva* kilisababisha neno *eng'ombe* kuamilisha theta ya shamirisho lakini baada ya uhamisho liliamilisha dhima ya kiima. Jambo hili halifai kwani kanuni dhima inasisitiza kuwa kila dhima hubeba theta maana moja tu. Hii ndiyo sababu kanuni theta inadhihirisha kuwa kitenzi tenda hakiwezi kuandikwa kama kauli tendwa.

Sentensi ya 4.20 (a) *Eng'ombe yakwivwa* 'ng'ombe imeibwa'. Tukichukulia kuwa '*eng'ombe*' ni shamirisho la *kwiva* na imehamishwa kuenda juu kwa namna rudilifu

kuwa kwanza kiima cha kauli tendwa *ivwa* 'ibwa' kisha kuwa kiima cha kibainishi *yaku* 'ime'.

Mwanzo inaweza kudhihirika kuwa sentensi hii haiafikiani na kanuni theta kwani 'eng'ombe' inaacha kuwa kiima cha *kwivwa* 'ibwa' na kuwa kiima cha *yakwivwa* 'imeibwa'. Kulingana na Chomsky 1981, kauli tendwa huamilisha dhima shamirisho zake lakini sio kiima. Yaani kiambishi tamati 'w' huchukua dhima ya kiima hivyo basi huondoa dhima ya kiima katika kauli tendwa (Hili huondolea kauli tendwa uwezo wa kuamilisha theta kiima). Hivyo basi theta maana ya pekee ambayo 'eng'ombe' inapewa ni ile ya shamirisho. Tunaona kwamba kuandika kwa kauli tendwa kunarahisishwa kwani kauli tendwa hakuamilishi theta kiima. Hili linatufanya tujiulize maswali zaidi, yaani ni nini kinachosababisha uhamisho wa dhima ya mtendwa? Hili husababishwa na kanuni ya kimofolojia ambapo kijenzi husonga tu ili kutosheleza umbo lake la kimofolojia jinsi itakavyojadiliwa katika kanuni ya ulafi.

### 4.2.6 Kanuni ya Ulafi

Kanuni hii ya ulafi huchunguza namna ambavyo viwakilishi hutumiwa katika sentensi. Kwa mfano:

(4.22) (a) *Oyo yamrora oyo*

Yeye alimuona yeye

*Oyo* 'yeye' ya kwanza ni kiima hivyo basi ina sifa za kiwakilishi cha nafsi ya kwanza na *oyo* 'yeye' ya pili inachukua mahala pa nafsi ya tatu. Katika Kimaragoli, badala ya 'oyo' ya nafsi ya tatu kiambishi (-m-) hutumiwa. Sifa za viwakilishi lazima

zichunguzwe kwa makini hasa wakati wa uundaji wa sentensi. Tazama sentensi ifuatayo:


(b) *Oyo yarora / na oyo*

Yeye aliona / na yeye

Katika sentensi hii *oyo* 'yeye' imetumiwa kama shamirisho ya kitenzi tenda *rora* 'ona'. *Oyo* 'yeye' haiwezi ikatumiwa kama shamirisho ya kitenzi tendwa *rorwa* '-lionwa'. Hivyo basi kauli tendwa ya *–rorwa* '-lionwa' huondoa uwezo wa kitenzi *–rora* '-ona' kuchunguza nafsi ya tatu. Tazama mchoro ufuataao:

Mchoro huu unatudhihirishia uhamisho ambapo yeye huchukua nafasi ya kiima na kibainishi ni dhahania. Hili linaeleza kuwa 'oyo' ilihamishwa tu kwa kuzingatia kanuni ya kimofolojia.

(4.23)



Mchoro huu unatudhihirishia uhamisho ambapo yeye huchukua nafasi ya kiima na kibainishi ni dhahania. Hili linaeleza kuwa 'oyo' ilihamishwa tu kwa kuzingatia kanuni ya ulafi.

**Hitimisho**

Sura hii imejadili namna ambavyo dhima tatu muhimu zinazoathiri sintaksia huhamishwa. Dhima hizi ni kiima na shamirisho lakini zenye theta maana ya mtenda, mtendwa na mhisi. Sehemu hii imetudhihirishia kuwa uhamisho hautokei tu kiholela bali huongozwa na kanuni mahsusi zifuatazo; kanuni ya athari, uhusiano wa kimuundo katik ya vijenzi tawala, kanuni ya uhamisho kwa masafa mafupi, kanuni theta kanuni ya ulafi na kanuni arifishi. Kanuni hizi huingiliana ili kusababisha kuwepo kwa uhamisho kwa namna wekevu zaidi.

Uhamisho wa dhima ni muhimu kwa sababu umetubainishia wazi kuwa lugha ya Lulogooli huongozwa na kanuni bia sawa na lugha nyinginezo kama vile Kiingereza na Kiswahili. Hili linatuonyesha kwamba uhusiano wa vijenzi vya sentensi na kanuni zinazotawala uundaji wa sentensi hutokea katika sintaksia ya lugha zote za binadamu. Pia ni wazi kuwa kuna uhusiano wa kipekee kati ya mofolojia na sintaksia, jambo lililoelezwa zaidi kwa kuzingatia kauli tendwa.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## Kitangulizi

Utafiti huu ulitekelezwa ili kueleza uhamisho wa dhima katika sentensi za Lulogooli kwa mtazamo wa sintaksia finyizi. Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha wazi kanuni zinazotawala uhamisho huu na kueleza muundo wa sentensi baada ya uhamisho. Hili ni dhihirisho kuwa dhima zinazopatikana katika sentensi hutegemea ni kiarifu kipi kilichotumiwa.

Nadharia hii inaendeleza imani kuwa sintaksia ni kitengo msingi zaidi cha muundo wa kisarufi. Inatambua hatua tatu muhimu ambazo ni:

(i) Idadishi kupitia majopo ya kisarufi

(ii) Uhamisho wa maumbo hayo

(iii) Muungano wa maumbo na kadhalika.

Sentensi sahili za Lulogooli zilikusanywa na kuchanganuliwa kwa kufanya majaribio kuona namna ambavyo dhima hizi hutokea na miundo yake baada ya uhamisho. Utafiti huu umeeleza vijenzi vya sentensi za Lulogooli, dhima zinazojitokeza na uhamisho wao. Sura hii itaeleza muhtasari wa matokeo ya utafiti na hitimisho. Dhima zimejadiliwa kuonyesha uamilishi wao katika sentensi. Kiarifu ndicho hutambulisha dhima hizi, kiima na aina mbalimbali za shamirisho zimeshughulikiwa ili kudhihirisha mahusiano yao na pia kueleza namna uhamisho wao unavyotokea.

## 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umeeleza na kudhihirisha muundo wa sentensi sahili za Lulogooli. Muundo wa kisintaksia wa sentensi hutawaliwa na kanuni bia ambazo ni utegemezi muundo, ufungami, ufasili kamili na kanuni leksia, ile bayana zaidi inayotokeza ni ya upatanisho wa kisarufi. Kanuni hizi zimeongoza sentensi zote zilizojadiliwa katika utafiti huu.

Uchanganuzi wa sentensi za Lulogooli unadhihirisha kuwa sentensi hizo huundwa kutokana na mojapo ya maneno kisarufi. Maneno hayo yanaweza kuwa maneno leksia au amilishi. Maneno leksia huhusisha mojopo ya maneno kama vile, nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi na vuhusishi na virai vyao. Maneno amilishi huhusisha vibainishi, shamirisho na viunganishi. Ni wazi kuwa mojopo haya lazima yahusiane vizuri kwa kufuata sheria za uundaji wa sentensi ili kuunda sentensi sahihi.

Muundo wa virai vya Lulogooli umejadiliwa. Imedhihirika kuwa virai vimeundwa kutokana na maneno leksia. Maneno haya huungana na lile neno tawala ndilo huunda kirai husika. Virai leksia ni vitano ambayo ni kirai nomino, kirai tenzi, kirai kivumishi, kirai kihusishi na kirai elezi. Virai amilifu ni vitatu: kirai kiunganishi, kirai bainishi na kirai shamirisho. Virai leksia na virai amilifu huungana ili kuunda virai vikubwa zaidi ambavyo ni sentensi. Miundo ya sentensi hutegemea virai vilivyotumiwa katika kuziunda, kuna sentensi sahili, ambatano na changamano.

Uhamisho wa dhima hizi umeelezwa na kudhihirishwa namna unavyotokea kwa kutumia michoro matawi. Imedhihirika kwamba uhamisho wa dhima mbalimbali katika sentensi za Lulogooli huathiri muundo wa sentensi kwa jumla. Kila uhamisho huacha hamishe inayotambulika kisintaksia. Dhima yoyote ile lazima isonge tu hatua chache

kutoka pahala pa chini hadi kwa namna rudilifu. Pia kwa kuzingatia kanuni arifishi. Kanuni nyinginezo zinazojitokeza ni kanuni ya ufungami, ulafi na kanuni hamishe na kanuni theta.

Ni bayana kuwa vijenzi mbalimbali hufungamanishwa kimuundo kwa pronomino zake, hili limeelezwa kwa kuzingatia kanuni ya ufungami. Namna tujuavyo kiarifu ndicho msingi wa sentensi, hivyo basi uhamisho hutekelezwa hatua chache kutoka pahala pa chini hadi juu namna ilivyoelezwa na kanuni ya uhamisho kwa masafa mafupi. Uhamisho ambao hutekelezwa kwa namna rudilifu. Baada ya uhamisho sharti pawepo na hamishe jinsi ilivyojadiliwa na kanuni hamishe. Kihamisho huhamishwa kwa kuzingatia kanuni arifishi hutaka kila kiarifu kiwe na kiima.

Ili uhamisho utekelezwe kwa namna inayofaa lazima dhima ipewe theta moja tu. Iwapo dhima moja itapewa theta zaidi ya moja basi muundo wa sentensi utaathiriwa. Haya yameelezwa kwa kuzingatia kanuni theta. Sentensi za kauli tenda na tendwa zimeangaziwa kueleza bayana jambo hili kauli tendwa huamilisha theta shamirisho zake lakini sio kiima kwani kiambishi tamati [w-] huchukua dhima ya kiima, hivyo basi huondoa uwezo wa kauli tendwa kuamilisha theta kiima.

Kanuni ya ulafi imeangazisha zaidi namna ambavyo viwakilishi hutumiwa katika sentensi na athari zake katika kauli tenda na tendwa. Kijenzi cha sentensi husonga tu ili kutosheleza mahitaji ya umbo lake la kimofolojia, kwani hili lisipozingatiwa huenda kusiweko na sentensi sahili. Ni dhahiri kwamba uhamisho wa dhima hizi hutokea kuwa sawa isipokuwa tofauti kidogo hutokea kwenye sentensi ambazo zina vitenzi katika kauli tendwa ambapo dhima mbili hutosheleza majukumu sawa yaani huweza kuwa

kiima cha kiarifu katika kauli tenda na dhima hiyo pia iwe shamirisho katika kauli tendwa.

## 5.2 Mahitimisho ya Utafiti

Kutokana na muhtasari huu kuna mambo kadhaa ambayo tunaweza kuhitimisha tukiangazia lugha ya Lulogooli. Lulogooli huongozwa na kanuni kama tu lugha nyinginezo. Imedhihirika pia kuwa kanuni zinazotawala uhamisho zinaweza kutumiwa katika baadhi ya sentensi wala sio zote. Hili linamaanisha kuwa utaratibu na uamilifu wa sentensi hutawaliwa na kanuni mahsusi. Hivyo basi, tunaweza kuhitimisha kuwa mtazamo wa sintaksia finyizi unaweza kutumiwa kuchanganua sentensi za Lulogooli kwa ukamilifu.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Kazi hii imechunguza tu uhamisho dhima wa sentensi za Lulogooli. Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kubainisha ikiwa kunaweza kuwepo na uhamisho mwingine katika Lulogooli kama vile, vichwa na viulizi kwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi. Vile vile, uhamisho katika lugha nyinginezo unaweza kufanywa ili kueleza iwapo kuna tofauti yoyote. Hili litachangia katika kuendeleza uwanja wa sintaksia kwa misingi ya kinadharia. Isitoshe utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kubainisha bayana vibainishi na vipatanishi kwani suala hilo limejitokeza katika utafiti huu lakini halikushughulikiwa kwa undani. Masuala haya yakitiliwa maanani na kufanyiwa utafiti yataondoa utata uliopo baina ya vijenzi hivi viwili miongoni mwa lugha mbalimbali za Kiafrika.

Utafiti huu umeeleza utaratibu wa uhamisho dhima katika sentensi sahihi za Lulogooli, kanuni zinazotawala uhamisho huo na maumbo yanayotokea pia yameshughulikiwa.

Hili limedhihirisha bayana kuwa kila uhamisho huongozwa na kanuni mahsusi bali hautokei tu kiholela. Utafiti huu utachangia katika kukuza na kuendeleza uwanja wa Sintaksia katika lugha za Kiafrika kwa misingi ya nadharia za kisasa. Aidha, utachangia katika kueleza ubia na umahsusi wa lugha hizi kwa kuzingatia kanuni mwafaka zinazowatala uundaji na uhamisho wa dhima.

## MAREJELEO


Adagala, K. 1979: Language and Literature in Primary Schools: Lulogooli ne Tsing'ano Tsya Valogooli: University of Nairobi, Institue of African Studies, Discussion Paper No. 121

Adagala, K. 1979: Language and Literature in Primary Schools; Lulogooli ne Tsing'ano Tsya Valogooli: M.A. Thesis (Unpublished) University of Nairobi.

Atkinson, M. 1996: *The Minimalist Program:* Concise Encyclopaedia of Syntactic Theories: (eds) Brown, K na Miller, J. Edinburgh: Pengamon Press.

Chomsky, N. 1965: *Aspects of the Theory of Syntax:* Cambridge: Massachuessette Institute of Techonology Press.

Chomsky, N. 1995: *The Minimalist Program:* Cambridge: Massachuessette Institute of Techonology Press.

Chomsky, N. 1996: Some Observations on Economy in Generative Grammar: Cambridge: Massachuessette Institute of Techonology Press.

Cook, V. J. 1988: *Chomsky's Universal Grammar:* Oxford, Basil Blackwell.

Cook, V.J. and Newson 1996: *Chomsky's Universal Grammar:* 2nd edition. Oxford, Basil Blackwell.

Frawely, W. J. 2003: *International Encyclopedia of Linguistics:* New York: Oxford University Press.

Gachukia, E. W. *et al* 1968: *Isindu ne Ingida Yeye.* TKK Supplimentary Reader 2: Lulogooli, Nairobi, Longman.

Habwe, J. na Karanja P. 2002. *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*: Nairobi, Phoenix Publishers.

Kawa, A. N. 2003: The Syntax of Noun Phrase Movement in Kiswahili: M. A. Thesis (Unpublished), Kenyatta University.

King'ori A. 2005: Movement in the Kiswahili Sentence: A Minimalist Approach: M. A. Thesis (unpublished), Kenyatta University.

Lidonde, A. M. 1978: A Generative Phonology of Lwitakho: A Luhya Dialect: M.A.Thesis,University of Nairobi

Lugadiru, J. *et al* 1968: *Afandi na Kaana Keke:* TKK Supplimentary Reader 1: Lulogooli, Nairobi, Longman.

Lugadiru, J. *et al* 1970: *Engoko Yagoota:* TKK Supplimentary Reader 1: Lulogooli, Nairobi, Longman

Lugadiru, J. *et al* 1971: *Lisoosa Lyokutwekitsa Muhiga;* TKK Supplimentary Reader 3: Lulogooli, Nairobi, Longman.

Nyaga, S. W. 1998: A Syntactic Analysis of the Ki-embu Simple Sentence: A Governement and Binding Approach: M. A. Thesis (unpublished): University of Nairobi.

Palmer, F.R. 1994: *Grammatical Roles and Relations:* New York, Cambridge University Press.

Poole, G. 2002: *Syntactic Theory:* Hampshire, Palgrave

Radford, A. 1997: *A Syntax: A Minimalist Introduction:* Cambridge, Massachuessette Institute of Techonology Press.

Samba, Z. K. 1988. Lugooli, Wanga and Lubukusu dialects of Luhyia: A Study of Major Phonological Processes; M.A. Thesis, (Unpublished) University of Nairobi.

Wasike, A. K. 1992: The Lubukusu Simple Sentence: Government and Binding Approach: M. A. Thesis (unpublished): University of Nairobi.

## KIAMBATISHO

**Sentensi za Luloogoli**

1. *Juma amkuyi Yohana*

   Juma alimchapa Yohana.

2. *Umwana akungi imbwa.*

   Mtoto alifukuza mbwa.

3. *Umwana agona.*

   Mtoto analala.

4. *Umwana akubi likele.*

   Mtoto alipiga chura.

5. *Juma akina.*

   Juma anacheza.

6. *Guga avoha eng'ombe.*

   Babu anafunga ng'ombe.

7. *Guku yadekera guga ovosera.*

   Nyanya alimpikia babu uji.

8. *Umwigitsi azii ku mudoga.*

   Mwalimu ameenda kwa gari.

9. *Tsing'ombe tsilitsa maduma mumulimi.*

   Ng'ombe wanakula mahindi shambani.

10. *Uvuyanzi avana vadi.*

    Uwapende watoto wadogo.

11. *Vayanzwi avana vadi.*

    Wapendwe watoto wadogo.

12. *Vosi vakina mukiguti.*

Wote wanacheza uwanjani.

13. *Avasomi vagumirwi.*

Wanafunzi washikwe.

14. *Imali yanyagura yengo vwangu.*

Imali alikimbia nyumbani haraka.

15. *Umwigitsi yatsi musikulu.*

Mwalimu alikuja shuleni.

16. *Mama yatsa yengo.*

Mama alikuja nyumbani.

17. *Eng'ombe yakwirwa.*

Ng'ombe imeibwa.

18. *Oyo yamrora oyo.*

Yeye aliona yeye.

19. *Oyo yarora/na oyo.*

Yeye aliona/na yeye.